

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MIKUTANO WA KWANZA

Kikao cha Tatu – Tarehe 12 Novemba, 2020

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaweza kukaa.

Waheshimiwa Wabunge, karibuni sana. Natumaini kupitia *tablets* zenu kila mmoja ameshaiona *Order Paper* ya leo yaani Orodha ya Shughuli za leo ambazo ni muhimu sana. Tutaanza na Kiapo cha Uaminifu kwa Waheshimiwa Wabunge ambao bado hawajaapa. Tuna Wabunge wanne wa ACT-Wazalendo na Mbunge mmoja wa Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Bado sina hakika kama Wabunge wa ACT wapo, lakini sisi tutawataja kama utaratibu ulivyo hapa. Kama watakuwepo, basi tutawaapisha. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ajenda itakayofuata ni uthibitisho ambao mtapaswa kuufanya kwa uteuzi wa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, nawaomba Wabunge ambao wako nje au *canteen* na wapi, basi waingie ndani na ninyi mlioko ndani msitoke kwa sababu jambo hili ni kubwa na mkononi sina hilo jina hivi sasa, sina kabisa. Wakati ukifika basi Mpambe wa Mheshimiwa Rais tutamruhusu aingie hapa ndani na bahasha husika na nitakabidhiwa hapa mbele yenu. (*Makofi*)

Candidates ni ninyi wote, kwa hiyo, kila mtu akae sawa, isipokuwa mimi na AG. Maana yake mliobaki wote ni ma-candidate. Sasa usije ukatuuangukia hapa, aah! Halafu itakuwa taabu. Tunawatakia kila la heri wote muweze kuteuliwa. (*Kicheko/Makofi*)

Baada ya hapo tutakuwa na Uchaguzi wa Mheshimiwa Naibu Spika na pia tutakuwa na Kiapo cha Mheshimiwa Naibu Spika. Baada ya hapo tutaelezana mambo mengine yanayoendana na hayo.

Basi, tuanze haya mambo. Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

KIAPO CHA UAMINIFU KWA WABUNGE

(Kiapo Kinaendelea)

355. Mhe. Rose Cyprian Tweve

(Mbunge Aliyetajwa Hapo Juu Aliapa Kiapo cha Uaminifu)

SPIKA: Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

KUTHIBITISHA UTEUZI WA WAZIRI MKUU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa jambo hili ni zito, nahitaji kupumua kidogo. (*Kicheko*)

Pia inabidi niwatume watu wangu waangalie angalie katika viunga vya Bunge kama Mpambe wa Mheshimiwa Rais (*ADC*) atakuwa ameshafika katika viwanja hivi na tufanye maandalizi ya kumleta humu ndani. Kwa jinsi hiyo, ili nanyi mkae sawa, basi nasitisha shughuli za Bunge kwa muda wa nusu saa hivi halafu wote tuwe tumerudi mahali petu.

Naomba kusitisha Shughui za Bunge kwa muda wa nusu saa. Maaskari wameenda likizo?

(*Saa 3.10 Asubuhi Bunge lilitishwa hadi saa 3.40 asubuhi*)

(*Saa 3.47 Asubuhi Bunge lilirudia*)

SPIKA: Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

KUTHIBITISHA UTEUZI WA WAZIRI MKUU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama inavyoonekana kwenye Orodha ya Shughuli za Bunge ya leo tarehe 12 Novemba, 2020 Bunge lina kazi ya kuthibitisha uteuzi wa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ibara ya 51(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inaeleza kwamba, minanukuu; "Mapema iwezekanavyo, na kwa vyovoyote vile ndani ya siku kumi na nne, baada ya kushika madaraka yake, Rais atamteua Mbunge wa kuchaguliwa kutoka katika Jimbo la Uchaguzi anayetokana na chama cha siasa chenye Wabunge wengi zaidi Bungeni au kama hakuna chama cha siasa chenye Wabunge wengi zaidi, anayeelekea kuungwa mkono na Wabunge walio wengi kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano, naye hatashika madaraka hayo mpaka kwanza uteuzi wake uwe umethibitishwa na Bunge kwa azimio litakaloungwa mkono na kura za Wabunge walio wengi." Mwisho wa kunukuu. (*Makofii*)

Hayo ndio maelezo ya Katiba yetu. Aidha, Kanuni ya 31 ya Kanuni za Bunge, Toleo la Juni, 2020 linaainisha utaratibu utakaofuatwa na Bunge katika kutekeleza jukumu hilo la Kikatiba la kuthibitisha uteuzi wa Waziri Mkuu. Utaratibu huo kwa ujumla wake unahusisha matukio makuu yafuatayo:-

Tukio la kwanza, Mpambe wa Rais kuingia ndani ya Ukumbi wa Bunge na kumkabidhi Spika bahasha yenye

Taarifa ya Rais inayotaja jina la Mbunge anayependekezwa kuwa Waziri Mkuu. (*Makof*)

Pili, Spika kuwasomea Wabunge taarifa hiyo na kulitaja jina la Mbunge anayependekezwa na Rais kuwa Waziri Mkuu. (*Makof*)

Tatu, Bunge kusitishwa kwa muda ili kumpa nafasi Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuandaa wasifu wa Mbunge anayependekezwa kuwa Waziri Mkuu na Azimio la Kuliomba Bunge Kuthibitisha uteuzi huo na pia kutoa nafasi kwa Katibu wa Bunge kukamilisha uwekaji wa jina la Mbunge huyo kwenye karatasi za kura. Yaani hapa maana yake ni kwamba kwa sababu hatuna jina mpaka sasa hivi, isingekuwa rahisi kwa Katibu wa Bunge kutengeneza karatasi ya kupigia kura. Kwa hiyo, tutakapositisha kwa muda, inampa nafasi Katibu kufanya hilo.

Pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali hapo alipo hana jina la Waziri Mkuu anayependekezwa. Kwa hiyo, tutasitisha kwa muda kidogo ili akatengeneze wasifu na aandae Azimio ambalo litatusaidia sisi kuliamua Azimio hilo kwa kupiga kura ndani ya Ukumbi huu wa Bunge.

Baada ya kusitisha kwa muda mfupi ili Mwanasheria Mkuu na Katibu wa Bunge wafanye majukumu yao hayo, tutakaporejea Mwanasheria Mkuu wa Serikali atatoa hoja ya kuliomba Bunge lithibitishe uteuzi wa Mbunge husika kuwa Waziri Mkuu Mteule kwa kusoma Azimio husika na kumalizia kwa maneno "Naomba kutoa hoja."

Waheshimiwa Wabunge watasmama kuunga mkono hoja hiyo; na kwa taratibu zetu, Wabunge wachache wanaweza kuunga mkono kwa kuongea.

Kura za siri zitapigwa na baada ya kuhesabiwa kura hizo, Katibu wa Bunge atamkabidhi Spika matokeo ya kura hizo ili Spika aweze kuyatangaza.

Mwisho, baada ya Waziri Mkuu Mteule kuthibitishwa na Bunge, anaweza kupewa nafasi ya kutoa neno la shukrani kwa Wabunge; na hapo shughuli ya kuthibitisha uteuzi wa Waziri Mkuu itakuwa imekamilika. Huo ndiyo utaratibu.

Ukimya huu unanitisha! Waheshimiwa mmenyamaza kweli kweli! (*Makofi/Kicheko*)

Kwa jinsi hii Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo yangu hayo ya ufasaha kabisa, sasa namuagiza *Sergeant-At-Arms* amuingize ndani ya Ukumbi wa Bunge, Mpambe wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili tuanje shughuli yetu. (*Makofi*)

*Hapa Mpambe wa Rais (Kanali Bernard Mlunga) Aliingia
Ukumbini kuwasilisha jina la Mbunge aliyeeteuliwa na Rais
kuwa Waziri Mkuu*

SPIKA: Makofi hayo hayatoshi. (*Makofi*)

KANALI BERNARD MLUNGA - MPAMBE WA RAIS:

Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Job Ndugai, nimeagizwa kwako na Rais na Amiri Jeshi Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kuwasilisha *document* kwako.

Kwa heshima na taadhima, sasa naomba niwasilishe. (*Makofi*)

*(Hapa Spika alipokea bahasha iliyokuwa na jina la
Mbunge aliyeeteuliwa na Rais kuwa
Waziri Mkuu)*

SPIKA: Katibu wa Bunge, naomba uje. (*Makofi*)

Natumaini Waheshimiwa Wabunge wote mnaona bahasha hii. Huku nyuma iko *sealed* kabisa, ina mihuri sita ya siri. Kwa hiyo, iko *intact*jamani. Mpambe ameifikisha kama iliviotakiwa, salama kabisa. (*Makofi*)

Basi nimpe Katibu wangu afanye kazi ya kuifungua.
(Makofi)

*(Hapa Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai alifungua
bahasha iliyokuwa na jina la Mbunge aliyeteuliwa kuwa
Waziri Mkuu)*

SPIKA: Eh! Naona ziko mbili. Zote zina *signature* ya Mheshimiwa Rais. Sasa hii moja kwa niaba yenu, Mpambe hawezি kurudi tu hivi hivi, lazima nikiri kupokea. *(Makofi)*

Mbele yenu Waheshimiwa namkabidhi Mpambe wa Rais. *(Makofi)*

*Hapa Mpambe wa Rais (Kanali Bernard Mlunga) alimuaga
Spika kwa saluti na kuondoka Ukumbini baada ya
kumkabidhi Spika bahasha iliyokuwa na jina la
Mbunge aliyeteuliwa kuwa Waziri Mkuu*

MBUNGE FULANI: Koh oh! Mh, Mh! *(Kicheko)*

SPIKA: Barua hii ikitoka kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikielekezwa kwangu kama Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inahusu uteuzi wa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Imeandikwa ifuatavyo:-

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 51(2), Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya kushika madaraka yake, ndani ya siku 14, atamteua Mbunge wa kuchaguliwa kutoka katika Jimbo la Uchaguzi anayetokana na chama cha siasa chenye Wabunge wengi zaidi au kama hakuna chama cha siasa chenye Wabunge wengi zaidi, basi atateuliwa anayeelekea kuungwa mkono na Wabunge wengi kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hata hivyo, Waziri Mkuu atakayeteuliwa hatashika madaraka hayo hadi uteuzi wake uwe umethibitishwa na Bunge kwa azimio litakaloungwa mkono na kura za Wabunge walio wengi.

Hivyo, kwa kutekeleza matakwa hayo ya Katiba, nimemteua Mheshimiwa... (*Makofi/Kicheko*)

Naomba nirudie hapo, Mheshimiwa Rais anasema, anatuambia sisi Wabunge, hivyo, kwa kutekeleza matakwa hayo ya Katiba nimemteua Mheshimiwa Mbunge wa Ruangwa, Kassim Majaliwa... (*Makofi/Vigelegele*)

(Hapa Wabunge walimzunguka Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa huku wakimshangilia na kumpongeza)

SPIKA: Waheshimiwa naomba mumpishe Waziri Mkuu pendekezwa ili aje kwenye kiti chake hapa. Naomba tutoe njia hapo na Waheshimiwa wapambe tumsindikize Mheshimiwa Waziri Mkuu tumlete hapa mbele. (*Kicheko*)

Tusimzuie njia tumpishe hapo. Tumsogeze angalau awe viti vya mbele hapa. (*Makofi/Vigelegele*)

WABUNGE FULANI: CCM! CCM! (*Makofi/Vigelegele*)

(Hapa Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa alikaa kwenye kiti chake)

SPIKA: Ahsante sana, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tukae.

Kwa hiyo Mheshimiwa Rais ameleta jina la Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Mbunge wa Ruangwa, ili uteuzi wake uthibitishwe na Bunge tukufu kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi/Vigelegele*)

Sasa tunaendelea na utaratibu ule ambao nilikuwa nimeuainisha hapo mwanzo ambapo nitamuomba sasa

Katibu asome maelezo ya hatua inayofuata. Katibu wa Bunge tafadhalii.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yako ya awali, naomba sasa usitishe Bunge kwa muda ili Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali aweze kuwasilisha Azimio la Serikali.

SPIKA: Ahsante sana Katibu wetu.

Sasa nasitisha Shughuli za Bunge kwa muda mfupi. Msiende mbali sana, lakini mnawenza mkaapata chai kidogo katika maeneo yetu ya Bunge ili Mwanasheria Mkuu wa Serikali aweze kufanya kazi ya kuandaa wasifu na azimio ambalo tunakuja kulifanyia kazi muda si mrefu.

Naomba sasa nisitishe Shughuli za Bunge hadi muda mfupi ujao. Waheshimiwa Wabunge, naomba tusimame.

*(Saa 4.04 Asubuhi Bunge lilitishwa ili kumpa nafasi
Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuandaa wasifu wa Waziri
Mkuu Mteule ili kuuwasilisha Bungeni)*

(Saa 4.27 Asubuhi Bunge lilitrudia)

KUTHIBITISHA UTEUZI WA WAZIRI MKUU

MHE. PROF. ADELARDUS L. KILANGI - MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwasilisha hoja ya Serikali kuhusu kuthibitisha Uteuzi wa Waziri Mkuu katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii kwa mujibu wa Kanuni ya 31(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la Juni, 2020, ili niwasilishe Hoja ya Serikali kuomba Bunge lako Tukufu limthibitisho Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyeulewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya

Muongano wa Tanzania kwa mujibu wa Ibara ya 51 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sura ya Pili ya Sheria za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kabla sijatekeleza jukumu hili la Kikatiba, naomba nianze kwa kumshukru na kumtukuza Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na karama mbalimbali na hivyo kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi kama tunavyomwomba kila siku ya Shughuli za Bunge, ambapo pamoja na mambo mengine katika dua yetu tunamwomba Mwenyezi Mungu aibariki nchi yetu idumishe uhuru, umoja, haki na amani.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa ushindi wa kishindo alioupata katika Uchaguzi Mkuu uliomalizika hivi karibuni ambapo alichaguliwa na kukabidhiwa dhamana ya kuongoza tena nchi yetu akiwa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miaka mitano ijayo; namtakia kila la heri katika uongozi wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda pia kutumia fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa kuniamini na kunitfea tena katika nafasi hii ya Mwansheria Mkuu wa Serikali. Nitaendelea kutekeleza majukumu yangu ya Kikatiba na kisheria kwa kuzingatia Katiba na Sheria za Nchi yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa viapo vyangu katika utumishi wa umma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa na wananchi wa Jimbo la Kongwa ili uwe Mbunge wao kwa kipindi kingine cha miaka mitano. Napenda kukupongeza pia kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Kumi na Mbili. Uzoefu na umahiri uliouunesha katika Bunge la Kumi na Moja katika kusimamia na kuendesha Shughuli za Bunge ndiyo uliotupa imani sisi Wabunge kukuchagua tena kura za kishindo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naungana na Wabunge pamoja na wananchi wa Tanzania kukutakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu ya kuongoza Mhimili huu wa Bunge kwa mafanikio.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuingia Bungeni; nawatakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yenu kwa umma huku mkizingatia na kuheshimu Katiba, Sheria na Kanuni za Kudumu za Bunge mnapokuwa mnatekeleza majukumu yenu kama wawakilishi wa wananchi kwa maslahi ya wananchi wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, sasa naomba kutoa hoja, kwa mujibu wa Kanuni ya 31(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2020, kuliomba Bunge lako lithibitisho uteuzi wa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliofanywa na Mheshimiwa Rais kwa mujibu wa Ibara ya 51 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 51(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina masharti yanayoelekeza kwamba Rais atamteua Mbunge wa kuchaguliwa kutoka katika jimbo la uchaguzi anayetokana na chama cha siasa chenye Wabunge wengi zaidi Bungeni au, kama hakuna chama cha siasa chenye Wabunge wengi zaidi, anayeelekea kuungwa mkono na Wabunge walio wengi kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwamba Mbunge atakayeteuliwa kushika wadhifa huo hatashika madaraka hayo mpaka kwanza uteuzi wake uwe umethibitishwa na Bunge kwa azimio litakaloungwa mkono na kura za Wabunge walio wengi.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo sasa wote tunafahamu, Mheshimiwa Rais amemteua Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa ni Mbunge wa kuchaguliwa kutoka Jimbo la Uchaguzi la Ruangwa na anatoka Chama cha Mapinduzi

ambacho kwa mujibu wa matokeo ya uchaguzi mkuu uliofanyika tarehe 24, Oktoba, 2020 na kutangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, ndicho chama chenye Wabunge wengi zaidi Bungeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile, kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 51(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais amelileta jina hilo la Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa katika Bunge hili Tukufu kwa ajili ya kuthibitishwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naamini kwa dhati Waheshimwa Wabunge mtakubaliana nami kwamba Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa ni mtu muadilifu, asiyekuwa na makuu na mwenye hekima na busara nydingi; msikivu wa hali ya juu na mchapakazi hodari anayemudu majukumu yake ipasavyo katika zama hizi za uwajibikaji. Ni mtu mwenye uwezo wa kuchambua kwa kina na kupima hoja mbalimbali zinapojitokeza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, aidha, umahiri wake katika kusimamia utendaji na kudhibiti nidhamu katika utumishi wa umma, mapambano dhidi ya rushwa na usimamizi bora wa sera za Taifa na uongozi bora wa Serikali katika utekelezaji wa Shughuli za Bunge umejidhihirisha katika uongozi wake kama Waziri Mkuu katika kipindi cha kwanza cha Awamu ya Tano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, utendaji mzuri na umahiri wa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa katika kazi yake kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita ulionekana pia katika nafasi yake kama Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria na Baraza la Mawaziri, Kamati ambayo ina jukumu la kupitia na kujadili kwa kina mapendekezo yote ya Miswada ya Sheria kabla ya Miswada husika kuwasilishwa Bungeni. Katika kipindi chake kama Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Miswada 60 ilifanikiwa kuwasilishwa Bungeni na hatimaye kupitishwa na Bunge kama Sheria za Nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri, Meshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa ni mzoefu katika nafasi ya Waziri Mkuu kwa kuwa ni nafasi aliyoitumikia kwa miaka mitano ya kipindi cha kwanza cha Awamu ya Tano. Kwa nafasi hiyo, yeye ndiye alikuwa kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. Naamini nyote mtakubaliana nami kuwa, aliitumikia nafasi yake kwa weledi mkubwa na hakusita kujibu maswali yote ya Wabunge na kutoa ufanuzi kwenye masuala mbalimbali yaliyohusu mipango ya utendaji wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha sifa hizi katika Bunge hili Tukufu ili kuonesha kwamba Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa ana uwezo wa kuyabeba na kuyahimili majukumu yote yanayoendana na wadhifa wa kazi na mamlaka ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama yalivyoainishwa chini ya Ibara ya 52(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sheria nyingine za nchi na hata Kanuni za Kudumu za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la Juni, 2020 ambayo ni:-

Kwanza, udhibiti, usimamiaji na utekelezaji wa siku hata siku wa kazi na shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano; Pili, kuwa Kiongozi wa Shuguli za Serikali Bungeni na; Tatu, kutekeleza jambo lolote ambalo Mheshimiwa Rais atamuagiza.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa kwa heshima na taadhima kubwa, naliomba Bunge lako Tukufu lithibitishe uteuzi wa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge wa Jimbo la Uchaguzi la Ruangwa, uteuzi uliofanywa na Mheshimiwa Rais, ili awe Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupitisha Azimio la Bunge. (*Makofii*)

Azimio lenyewe ni kama ifuatavyo:-

Azimio la Bunge la Kumthibitisha Waziri Mkuu chini ya Ibara ya 51(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kanuni ya 31(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

KWA KUWA Ibara ya 51(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inaeleza kwamba kutakuwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atakayeteuliwa na Rais kwa kufuata masharti ya ibara hii ambaye kabla ya kushika madaraka yake ataapa mbele ya Rais;

NA KWA KUWA Rais kwa mujibu wa Ibara ya 51(2) amemteua Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge wa Kuchaguliwa wa Jimbo la Uchaguzi wa Ruangwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania;

NA KWA KUWA Ibara ya 51(2) inaeleza kwamba Waziri Mkuu aliyyeteuliwa hatashika madaraka hayo mpaka kwanza uteuzi wake uwe umethibitishwa na Bunge kwa Azimio lilioungwa mkono na kura za Wabunge walio wengi;

HIVYO BASI, kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 51(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaazimia kama ifuatavyo:-

Kwamba Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge wa Kuchaguliwa kutoka Jimbo la Uchaguzi la Ruangwa na ambaye ameteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano, amethibitishwa na Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 31(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makof*)

MHE. WILLIAM V. LUKUVI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali; hoja imetolewa na imeungwa mkono na Wabunge wote. Nawashukuru sana na ahsante sana kwa kazi nzuri ambayo umeifanya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. (*Makof*)

Sasa nitaomba baadhi ya Wabunge wapate nafasi muda mfupi iwezekanavyo kuchangia hoja hii. Wabunge hao nitawaibua tu mimi mwenyewe; tuanze na Mheshimiwa Lukuvi, atafuatiwa na Mheshimiwa Kapteni Mkuchika na Mheshimiwa Mama Salma Kikwete ajiandae.

MHE. WILLIAM V. LUKUVI: Mheshimiwa Spika, naomba nirudie kukupongeza tena kwa kuchaguliwa na Bunge hili kuwa Spika wa Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na pumzi ambayo imeniwezesha kusimama hapa leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijaunga mkono hili azimio, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli, kwanza kwa kuchaguliwa kwa rekodi kubwa ambayo haijapata kutokea Rais anayegombea kipindi cha pili kupata uungwaji mkono wa namna hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, nampongeza sana pamoja na kuchaguliwa lakini kwa kazi kubwa aliyoifanya katika kipindi cha miaka mitano hii ambayo bila unafki, kazi ile aliyoifanya na Serikali ndiyo iliyotubeba sisi wote hasa Wabunge wa CCM kuja ndani ya Bunge hili. Ilikuwa rahisi kugombea na kusema tuna umeme kila kijiji, oneni hiki na hiki na tumefanikiwa wote kutokana na kazi kubwa iliyofanywa na Chama Cha Mapinduzi kwa hiyo, nampongeza sana (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la tatu nampongeza sana mtu wa Mungu huyu kwa maono yake. tunakumbuka kipindi 2015 aliletä jina la Mheshimiwa Majaliwa. Sisi tunamjua, tulikuwa naye hapa lakini wengi walikuwa wanasesma Majaliwa ni nani. Lakini kwasababu Mheshimiwa Rais mara nyngi mambo mengi anayoyafanya wakati mwingine unashangaa anayaafanya lakini anakuwa na Baraka za Mwenyezi Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, alipomchagua Mheshimiwa Dkt. Magufuli, wameendana sana, amem-tune vizuri na

amemsaidia sana, amelisaidia Taifa katika kutekeleza kazi za Serikali. Kinyume kabisa na watu walivyodhani. Mheshimiwa Dkt. Magufuli tunampogezza sana kwa maono yake. yako mengi ameyatabiri na yamekuwa tofauti kabisa katika Dunia hii, likiwemo la corona. Kwa hiyo, na hili nalo alilitoa na kusema kinyume na matarajio ya wengi. Lakini kumbe ndiyo mtu bora, bora kabisa ametuvusha katika kipindi cha miaka mitano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa maono hayo. Mheshimiwa Dkt. Magufuli amemteua Mheshimiwa Majaliwa katika miaka mitano bila unafki, nasema Mheshimiwa Majaliwa amefanya kazi kubwa sana katika miaka mitano hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza kama binadamu, Mheshimiwa Majaliwa ni binadamu mzuri sana. Unaweza ukamuona kama ana sura ya kuchukia akikaa peke yake, lakini akikaribiana na binadamu mwenzake huwezi kumuona amechukia. Jana nimeona watu wengi mmepiga naye picha, kama picha zenu mgezilinganisha hivi, mnaweza mkakuta wote mliopiga picha mna sura inayofanana na Mheshimiwa Majaliwa, nimekaa naye muda mrefu tangu akiwa Naibu Waziri, sijawahi kumuona huyu baba akikasirika. Hata kwa jambo unalofikiri kwamba jana tu labda nimemkwaza hivi, lakini ukifika kwake, meno kama yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Mheshimiwa Majaliwa naye amejaaliwa ana kipaji chake. Mungu amemtengeneza ni binadamu mwenye upendo, mchapakazi, mwenye huruma, hana majivuno. Kwa hiyo, tunaweza tukasema mengi lakini huyu baba ametembea kwa mara ya kwanza katika rekodi Waziri Mkuu katika kipindi cha miaka mitano anatembea mikoa yote na wilaya zote akiwa Waziri Mkuu. Sisi wote hapa asilimia zaidi zaidi ya ngapi ni Wabunge wa CCM, kwa mara ya kwanza tumeona Mjumbe wa Kamati Kuu akitembea. Sijawahi kuona! Niko kwenye Kamati Kuu miaka yote lakini sijawahi kumuona Mjumbe wa Kamati Kuu kama huyu ameruka kama kipepeo amekwenda kuwatetea

Wabunge zaidi ya asilimai 90 humu ndani. Sasa huu ni upendo wa namna gani? (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. WILLIAM V. LUKUVI: Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kuunga mkono hoja hii. Hoja hii ya Mheshimiwa Rais kwa kweli ametutendea haki Watanzania. Mheshimiwa Majaliwa anatosha sana kuwa Waziri Mkuu kwa jinsi alivyomsaidia Mheshimiwa Rais na ninaamini Waheshimiwa Wabunge wote tunamuunga mkono. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa William Lukovi. Sasa Mheshimiwa Kapt. (Mst.) George Mkuchika.

MHE. KAPT. (MST.) GEORGE H. MKUCHIKA: Mheshimiwa Spika, nami kwanza nikushukuru kunipa nafasi kuunga mkono hoja hii ya uteuzi wa Mheshimiwa Majaliwa aendelee kutuongoza kama Waziri Mkuu. Waheshimiwa Wabunge wenzangu, nimesimama hapa kuwarai, kuwaomba kura zote tumpigie Mheshimiwa Majaliwa. Nataka niseme Majaliwa namfahamu vizuri, nimefanya naye kazi Wizara ya Tawala za Mikoa, nimefanya nae kazi chini yake akiwa yeye Waziri Mkuu nikiwa Waziri. Nataka niwaeleze machache kama ninavyomfahamu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la kwanza nataka niseme hivi, hakuna mtu mstaarabu ninayemfahamu, anayeheshimu kila mtu, hajikwezi, hajipendekezi, anatenda haki kwa kila mtu kama Mheshimiwa Kassim Majaliwa. Waingereza wana msemo unaoashiria kwamba katika shughuli za Kibunge wengi wape lakini wachache wasipuuzwe, *minority should not be ignored.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie ndugu zangu, wale mliopo katika vyama mbali na CCM, muda wote Mheshimiwa Majaliwa alipotuongoza hapa ndani

hakubagua Wabunge katika utekelezaji wa shughuli za Bunge. Kwa hiyo, Wabunge wa vyama vingine mpeni kura Mheshimiwa Majaliwa mkiwa na uhakika kwamba atatenda haki, kama atakushughulikia wewe kama anavyomsghulikia Mbunge wa Newala Mjini, wa CCM. Ni mtu msikivu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninalotaka kusema kuhusu ndugu yangu Mheshimiwa Majaliwa kwamba ye ye kazi ya Waziri Mkuu tumeambiwa hapa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kusimamia uendeshaji wa shughuli za Serikali, Mheshimiwa Majaliwa katika kipindi chake kama Waziri Mkuu, amesaidia sana kusimamia kufufua uchumi wa nchi hii. Amesimamia sana mazao makubwa ya biashara, nilidhani ninamuona kwenye korosho tu, lakini nikamsikia yuko kwenye pamba, kahawa. Juzi amekwenda kufichua mdudu yallyokuweko Tanga, Mamlaka ya Mkonge ambapo ulibinafsishwa kinyume cha taratibu. Amerejesha mamlaka ya mkonge mikononi mwa Serikali na mazao mengine yote ameyashughulikia. Huyu ndiyo Mheshimiwa Kassim Majaliwa ambaye nimesimama hapa kuwarai Wabunge wenzangu tumuunge mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kama tulivyoelezwa hapa Waziri Mkuu kazi yake ni kusimamia uendeshaji wa shughuli za Serikali, anaratibu shughuli za Wizara zote, anaratibu kazi za Mawaziri wote walioko chini yake, wote tuliokuwa tunafanya kazi chini ya Mheshimiwa Majaliwa ametunyenyekea, hakuonesha kama ye ye ndiyo mkubwa, tumefanya naye kazi kwa ushirikiano mpaka tumetekeleza, tumefika hapa ambapo tumeifikisha nchi. Ninaomba tumpe kura zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine mwenzangu William hapa kasema. Mheshimiwa Majaliwa amefanya ziara kweli. Nchi hii ameitembelea na ameweza kumsaidia vizuri Rais kwasababu amejua kinachoendelea kila wilaya alifanya ziara katika mikoa alipo rudi amemshauri Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho nataka niseme leo michezo ni ajira maana yake mnaweza kuitangaza nchi yenu pia kwa upande wa michezo. Mheshimiwa Majaliwa ni mwanamichezo, pamoja na Uwaziri Mkuu wake, bado aliendelea kufundisha timu ya mpira ya Bunge. Hebu fikiria Waziri Mkuu, kocha wa mpira. Amesimamia shughuli za michezo katika nchi, sio ajabu kwamba katika kipindi hiki cha miaka mitano ya uongozi wa Rais Dkt. Magufuli na Waziri Mkuu akiwa Majaliwa, nchi yetu baada ya miaka 40 tulikuwa hatujashiriki mashindano ya kombe la Mataifa Huru ya Africa, lakini katika kipindi hiki, tumeshiriki. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, yametokea nini huko, lakini si mwanzo! Tukirudia tena mambo yatakuwa mazuri na tena na tena. Nimesimama hapa kuwaomba ndugu zangu...

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. KAPT. (MST.) GEORGE H. MKUCHIKA: Wabunge wenzangu wa vyama vyote tumuunge mkono Rais wetu kwa kumpigia kura za ndiyo Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa awe Waziri Mkuu wetu kipindi kingine cha miaka mitano. Nawashukuru. Ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mkuchika kwa maelezo yako mazuri kabisa na sifa nzuri ulizoviweka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu mpendekezwa. Nakushukuru sana, ahsante sana.

Mheshimiwa Mama Salma, atafuatiwa na Mheshimiwa kamishna, Fakharia Shomari. Fakharia yupo eh? Ahsante, utafuatia.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Spika, wetu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waheshimiwa Wabunge wote, kwanza naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa hii fursa ya kuweza kusimama kwenye Bunge lako tukufu kuweza kuzungumza machache ndani ya mengi ambayo hata tukizungumza ndani ya mwaka

mmoja hatuwezi kumaliza sifa alizokuwa nazo Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi kubwa na nzuri ambazo ameweza kuzifanya katika Taifa letu la Tanzania kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita. Kwa kweli ni kazi illyotukuka. Tanzania inajua, Afrika inajua na Dunia kwa ujumla inajua kwa kazi yake jinsi Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli alivyokuwa shupavu wa kusimamia yale ambayo watu walisema hayawezekani katika Afrika na hasa kwa Tanzania. Mheshimiwa Dkt. John Pombe ameyaweeza na ameionesha Dunia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru kwa kura nydingi alizozipata na tunamshukuru kwa kuwabeba Wabunge wote ambao leo hii wako kwenye Bunge hilli la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunakushukuru sana, tuko nyuma yako tunakuunga mkono. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunampongeza Mheshimiwa Rais wetu kwanza kwa kutuletea Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa kipindi kingine cha miaka mitano. Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa ninamfahamu, ninamjua na ninajua kazi zake. Hiki alichokionesha hapa Bungeni ni muendelezo wa kazi zake zilizotukuka. Mheshimiwa Majaliwa kwanza ni mnyenyeketu, pili ana heshima ambayo huwezi kuilinganisha, tatu hajikwezi ni mtu ambaye ameshuka mpaka chini. Ni mpole lakini si upole tu, ni upole unaoendana na ushupavu wa kusimamia mambo magumu na yakatekelezeka. Huyu ndiyo Mheshimiwa Majaliwa, tunayemfahamu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Majaliwa ni msimamizi wa shughuli za Serikali Bungeni. Katika kipindi cha miaka mitano, amefanya mambo mazuri, makubwa na yanayoonekana ndani ya Taifa letu la Tanzania. Hakuwa mbaguzi, watu wote ndani ya Bunge hilli la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliwaweka kuwa kitu kimoja bila kuangalia itikadi za vyama na watu ambao leo hii wamerudi

walishuhudia hata wale waliosema hapa, wanasema hapana hatuungi mkono hoja baada ya kumaliza upande huu tumeungwa mkono hoja, wote wanakimbia kwa Mheshimiwa Majaliwa, Mheshimiwa Majaliwa tunakuomba hili na hili na yeze aliwakaribisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachopenda kusema, Mheshimiwa Majaliwa tunampongeza kwa kuturejeshea lakini kikubwa alichokifanya yeze ana sifa zote zinazostahili, anastahiki kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Unastahili sana hakuna mtu anayeweza kupinga jambo hili.

SPIKA: Ahsante sana Mama, ahsante.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Umezunguka nchi nzima kuitetea llani ya Chama Cha Mapinduzi. Ninaunga mkono hoja, Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge hili kama si Majaliwa mwingine nani! Tumpe kura zote za ndiyo Mheshimiwa Majaliwa. Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza, tumpe kura zote za ndiyo kwa kazi alioifanya. Ahsante sana naunga mkono hoja. (*Makofii/Vigelegele*)

SPIKA: Ahsante sana. Maneno ya busara ya mama hayo. Mheshimiwa Fakharia, kifupi.

MHE. FAKHARIA SHOMARI KHAMIS: Mheshimiwa Spika, ahsante. Waheshimiwa Wabunge wenzangu, sina budi kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuletea neema ambayo leo imo ndani ya Bunge. Vile vile sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa vile kunijaalia kurejea tena Bungeni katika Bunge hili tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli tumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Amefanya uteuzi ambaao kwa mbali tulikuwa tunaufikiria lakini hatuwezi kuamua kama yeze mwenyewe hajatamka. Tushukuru amelitamka, Mheshimiwa Kassim Majaliwa kwetu sio mgeni, uwezo wa kazi anao, amefanya ziara ndani na nje ya Tanzania, Zanzibar na

Bara na ziara zake zimezaa matunda maana alikuwa anafanya ziara zenye mafanikio. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kassim Majaliwa alikuwa anafanya kazi na rika zote, alikuwa anafanya kazi na jamii yote na uwezo huo, kipaji hicho Allah Mungu alimbariki. Sasa kwakweli uliokuja hapa kwetu leo nawaomba Wabunge wenzangu, Wanzibar wenzangu tuibariki hii hoja ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano maana ye ye ndiyo Mheshimiwa Rais alizunguka Tanzania nzima na tumeona *percentage* yake aliyopata ya kura na baadhi yetu sisi tumeingia humu Bungeni kwa kura zake ye ye zilivyokuwa nydingi. Sasa kwa vyovyyote tunakupokea Mheshimiwa Kassim Majaliwa na tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa uteuzi wake alioutoa na uteuzi huu tumeukubali sote humu ndani na ninawaomba Wabunge wenzangu, hili jambo tunalibariki kwa umoja wetu na mafanikio yatakuwa kwetu sote na Watanzania kwa juma. Kwa haya machache, naunga mkono hoja na wenzangu wote wataunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa January Makamba, kifupi.

MHE. JANUARY Y. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nakupongeza kwa kuchaguliwa na watu wa Kongwa na namshukuru Mwenyezi Mungu kwa Baraka zake na rehema zake zilizotuwezesha wote kuwa hapa. Nawapongeza Wabunge wenzangu wote nanyi kwa kuchaguliwa kuja hapa Bungeni. Pia nimpongeze Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuendelea kuwa Rais wa nchi yetu, kura zake nydingi ni kielelezo cha imani kubwa walionyayo Watanzania kuhusu uongozi wake kwa yale aliyoyafanya na matarajio makubwa walionyayo kwake kwa miaka mitano ijayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, binadamu wanafahamika kwa namna tatu, kwanza anavyojifahamu mwenyewe, pili wanavyomfahamu wenzake na tatu anavyomfahamu Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Majaliwa anavyojifahamu, yeye hajatumia muda mrefu kutueleza kwamba yeye ni mtu wa namna gani, kwa sababu huwa hatumii muda mrefu kujisifu au kujielezea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunavyomfahamu sisi wenzake ambao tumefanya naye kazi, kwanza wanavyomfahamu watu wa Ruangwa, hata kumchagua kuwa Mbunge wao, maana yake ni kwamba wanamfahamu kwamba ni kiongozi hodari na mwenye uwezo na mchapakazi. Anavyomfahamu Mheshimiwa Rais, tunashukuru kwamba kwa uteuzi wa awali katika kipindi cha miaka mitano iliyopita na uteuzi huu, maana yake ni kwamba Mheshimiwa Rais anamfahamu Mheshimiwa Majaliwa kwamba ni kiongozi shupavu ambaye nafasi hii anaimudu na anaiweza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunavyomfahamu sisi Wabunge wenzake, maelezo yaliyotangulia yamejidhihirisha kwamba tunafahamu ni msikivu, ni mchapazi, mwadilifu na mnyenyeketu. Hakuna shaka yoyote kwamba nafasi hii ambayo Mheshimiwa Rais amemteua ndugu yetu, rafiki yetu Mheshimiwa Majaliwa anaimudu, anaiweza na ataitendea haki vizuri kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa anavyomfahamu Mwenyezi Mungu sisi hatujui, ila wanasema walatini "*vox populi, vox dei,*" yaani sauti ya wengi ni sauti ya Mungu. Kwa maelezo yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge walitangulia na kwa kura za watu wa Ruangwa na kwa uteuzi wa Mheshimiwa Rais maana yake ni kwamba *vox populi, vox dei* (sauti ya wengi ni sauti ya Mungu). Kwa maana yale tunayoyasema sisi na sifa tunazompa Mheshimiwa Majaliwa na tunavyomfahamu, basi bila shaka yoyote hata Mwenyezi Mungu anamfahamu hivyo. Kwa maana hiyo, uteuzi huu una baraka zote za Mwenyezi Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kiongozi yejote tangu Wafalme enzi na enzi, sifa zake zinajidhihirisha kwa namna mbili; ya kwanza, ni anayowatendea watu wake; ya pili, ni wale anaoamua wamzunguke na kumshauri. Sasa sifa za

Mheshimiwa Rais wetu zimejidhihirisha kwa yale aliyotutendea Watanzania kwa miaka mitano iliyopita na pia kwa uamuzi huu wa kumteua Mheshimiwa Majaliwa awe Mshauri wake Mkuu, awe Mtendaji Mkuu wa Serikali, asimamie shughuli za Bunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa sisi kumpigia kura nyingi za kumthibitisha ndugu yetu Mheshimiwa Majaliwa, tunafanya mambo mawili; kwanza, tunaonesha imani yetu kwa ndugu yetu, pia tunaonesha imani kwa busara ya Mheshimiwa Rais vilevile. Kwa hiyo, kura tutakayopiga hapa siku ya leo inatafsiri hizo mbili; ni kura ya imani kwa Mheshimiwa Majaliwa na pia ni kura ya imani kwa busara na hekima za Mheshimiwa Rais kwa uteuzi huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimalize kwa sababu muda ni mfupi kwa kumwomba Mwenyezi Mungu aendeleee kuibariki nchi yetu, aendeleee kumbariki Mheshimiwa Rais wetu, aendeleee kumbariki ndugu yetu Mheshimiwa Majaliwa na wasaidizi wote wa Mheshimiwa Rais watakaoteuliwa katika siku zijazo. Imani yangu ni kwamba sisi Watanzania Mwenyezi Mungu nchi ameibariki sana kwa yale yaliyopo ndani ya nchi yetu na ameibariki kwa busara kuu za viongozi wetu ambazo tunazitegemea sana ili nchi yetu iendelee kuwa na umoja, amani, utulivu na ipate maendeleo haraka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote, bila kuharibu kura hata moja, tuoneshe kweli kabisa kwamba tuna imani na Mheshimiwa Majaliwa, tuna imani na busara ya Mheshimiwa Rais na kwamba tunadhihirisha kwamba sauti yetu sisi kubwa na nyingi itatoa baraka kwa utendaji wa ndugu Mheshimiwa Majaliwa na Serikali hii kwa miaka mitano ijayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Kwa ajili ya muda, basi mchangiaji wetu wa mwisho kwa kifupi kabisa, awe ni Mheshimiwa David Silinde. (*Makofii*)

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii nami kuchangia hoja yetu kuu ya uteuzi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu pendekezwa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Kassim. Kwanza, tumpongeze kabisa Rais wetu, Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli kwa kumrudisha Waziri Mkuu wetu Mheshimiwa Kassim Majaliwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mengi yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge lakini mimi nitayasema kwa ufupi sana. Waziri Mkuu wetu Mheshimiwa Kassim Majaliwa moja ana uwezo wa kusimamia maono ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Magufuli kwenye kuibadilisha nchi yetu. Jambo la pilli kubwa ambalo lipo na litaendelea kuwepo kwa Mheshimiwa Kassim Majaliwa ni uwezo wake wa kuunganisha nchi yetu yote kupitia Bunge lako Tukufu na hivyo kufanya kazi ya Mheshimiwa Rais kuwa nyepesi katika kipindi chake cha miaka mingine mitano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sifa kuu ya kiongozi ni unyenyekevu, kujishusha na kusikiliza. Sifa hizo Mheshimiwa Kassim Majaliwa anazo. Kwa hiyo, kwa uwezo mkubwa alionao Mheshimiwa Kassim Majaliwa na kazi nzuri na maono na dira ambayo Mheshimiwa Dkt. Magufuli anayo kwa Taifa letu ninaamini sisi Wabunge wote siku ya leo tutampitisha Mheshimiwa Kassim Majaliwa kwa asilimia mia moja ili kuliambia Taifa nini tunakwenda kufanya kwa miaka mitano, baada ya miaka mitano ya mafanikio ambayo imeleta ushindi wa kimbunga ndani ya nchi yetu katika Uchaguzi Mkuu uliopita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, binafsi nampongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli na ninamshukuru kwa Mungu aliywongoza kuturudishia Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu pendekeza, Mheshimiwa Kassim Majaliwa. Ninaamini kabisa, bila wasiwasi wowote kwamba miaka hii mitano chini

ya Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli, chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa wanakwenda kufanya mabadiliko makubwa sana kwenye hili Taifa letu na bila shaka dunia inajua na watu wote wanafahamu kwamba hawa ni viongozi mahiri na kila mahali wanatetemeka kwa kusikia haya wanayoyafanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, niseme, wakati nikiwa katika Bunge la Afrika, mionganoni mwa viongozi waliokuwa wanasiwiwa na kila Mbunge kwenye Bunge la Afrika (*PAP*) walikuwa wanasesma Tanzania mna viongozi wenye maono ambao walistahili kupewa madaraka mara baada ya nchi zetu kuchukua uhuru. Sasa viongozi hao ni akina nani? Ni Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu na sasa pamoja na Mheshimiwa Kassim Majaliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naliomba Bunge Tukufu sisi wote kwa umoja wetu tumpitishie Mheshimiwa Kassim Majaliwa ili aweze kutuongoza tena kwa miaka mitano. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Nina hakika Waheshimiwa Wabunge wote mngependa kusema kitu, lakini muda hauko upande wetu itoshe tu kwamba walioongea wameongea kwa niaba yetu na maneno mazuri waliyoyasema kwa kweli kwa sasa yatoshe.

Katibu sasa tuendelee na hatua inayofuata, maelezo yako.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yako ya awali na Azimio la Serikali, sasa napenda kutoa utaratibu wa kupiga kura ya kuthibitisha uteuzi wa Waziri Mkuu kwa mujibu wa Ibara ya 51 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Kanuni ya 31(1)(2) na (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, kwanza kengele itapigwa kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge walio nje ya ukumbi kuingia ndani na wakati huo Waheshimiwa Wabunge watakuwa wanahesabiwa.

Baada ya Waheshimiwa Wabunge kuingia, kila mmoja atapatiwa karatasi ya kura yenyé jina la Mbunge anayependekezwa kuwa Waziri Mkuu na kila mmoja atatakiwa kuweka alama ya (v) kwenye chumba kilichopo mbele ya neno "ndio" au "hapana" kulingana na chaguo lake. Baada ya kura kupigwa, zoezi la kuhesabu kura litafuatia na hatimaye matokeo ya kura yatatangazwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya zoezi la kupiga kura na kutangazwa matokeo, Mheshimiwa Spika anaweza kumpa Mheshimiwa Waziri Mkuu Mteule fursa ya kusema maneno machache ya shukrani kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante sana. Kengele igongwe huko nje kwa ajili ya Mbunge ye yeyote ambaye yuko nje aweze kuingia ndani. Katibu natumaini watu wako wameshafanya *verification* ya idadi ya Waheshimiwa Wabunge walioko humu ndani ili tuweze kuendelea.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:
Mheshimiwa Spika, kwa sasa wako Wabunge...

SPIKA: Unaweza ukataja idadi?

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE: Ndiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa wako Waheshimiwa Wabunge 330 lakini baada ya kengele nina uhakika wataendelea kuingia. Kwa hiyo, tutakuwa tunaongezee idadi hii ambayo iko tayari.

SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile hatuna maswali, maana hakuna mgombea hapa, kwa hiyo, tunaenda moja kwa moja katika zoezi la kupiga kura. Naomba walioandalila sasa waje mbele na ma-box na karatasi. Kura hii ni muhimu sana kama alivyoeleza Katibu, unaweka alama yako ya (v) au *tick* kwenye ki-box cha ndiyo ili kuthibitisha uteuzi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Waheshimiwa Wabunge, hii ndiyo nafasi peke yake ambayo tumpewa Kikatiba ya *vetting*. Tunam-vet Waziri Mkuu. Jambo hili siyo la utani, ni jambo muhimu sana ambapo Bunge hili limepewa mamlaka haya makubwa ya kufanya hivyo. Mamlaka haya yanahashiria kwamba ninyi Waheshimiwa Wabunge pia siku moja ndani ya miaka mitano, ikitokea mmekasirishwa sana kwa sababu mnapiga kura leo ya kumwingiza Waziri Mkuu ofisini, huko mbele ya safari mkapiga kura ya kutokuwa na imani na Waziri Mkuu, maana yake ni kwamba Baraza la Mawaziri linakuwa limevunjwa.

Kwa hiyo, tujue tunachagua mtu ambaye ni muhimu kabisa, ndio Kiongozi wa shughuli zote za Serikali humu Bungeni, ndio mwenzetu anayetuwalilisha upande huo wa pili. Kama walivyosema waliotangulia, kwa kweli ni mtu ambaye atawasikiliza Waheshimiwa Wabunge wote wakati wote, usiku na mchana, anapatikana, ni mwenzetu miongoni mwetu. Basi tuendelee kupiga kura kwa haraka. Zile kura tayari zimepigwa, basi muanze kupita na ma-box mzikusanye, tusichukue muda.

Naomba kama mko wachache basi mwongezeko ili tuende haraka haraka. Hili zoezi la dakika mbili tatu tu, muanze kukusanya hizo kura. Anayegawa anakuwa mbele, anayekusanya yuko nyuma yake, twende *chap chap*. Ahsante sana. (*Kicheko*)

Tuendelee Waheshimiwa. Mnaogawa kura harakisheni mikono; kuweni wepesi. Tukusanye *chap chap*, zoezi la dakika chache sana. Mnaogawa karatasi, hebu changamkeni! Ukiishapiga tu basi weka kwenye *box* hapo ili

tuweze kuendelea. Leo mambo yetu ni mengi kidogo na tungependa ratiba yetu ikamilike kabla ya kuahirisha shughuli za Bunge mchana huu. mnaokusanya pia changamkeni *chap chap*. Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, hilo *box* unaweza ukaenda nalo upande huo pia ili uanze kukusanya. *Chap chap!* Waheshimiwa isichukue muda basi. Ahsante sana.

Muanze kuja, kama mtu bado ana kura anyooshe kura yake juu ili iweze kufuatwa kwa haraka na kukusanya. Haya njooni na *ma-box* hapa mbele msimame nayo hapo. Hakuna kura iliyobaki? Kuna hiyo moja inakuja huko nyuma. Aah, hakuna, zoezi limekamilika, wote tumepeiga kura. Bado! Msifanye masihhara. Ahsante sana.

Naomba Mheshimiwa Mariam Kisangi kwa niaba ya sisi wapiga kura tujiunge na timu ya kwenda kuhesabu. Mheshimiwa Mariam yuko wapi? Ehe, tafadhalii! Basi Waheshimiwa turuhusu timu ya Katibu iweze kwenda kufanya kazi hiyo na kutuletea majibu haraka iwezekanavyo. Haya wa *ma-box* mwende. Ahsante.

Wakati wanaenda kuhesabu kura naomba niwe na matangazo machache kama ifuatavyo:-

Kuna Mheshimiwa ambaye kwa bahati mbaya funguo zake amezipoteza pale getini wakati wa kuingia. Tunaomba kama una funguo ambazo siyo za kwako, basi uzilete hapa mezani badala ya kuzirudisha kule getini ili Mheshimiwa mwenzako asihangaike sana. Tuangalie kwenye mikoba yetu na *actually* tuwe makini kwenye mageti haya tunapopita kuhakikisha unachukua kitu kilicho cha kwako tu na usichukue kitu ambacho siyo cha kwako, inaleta usmbifu, miwani, funguo na vitu vya namna hiyo vinapotea mara kwa mara.

Pia hapo hapo kwenye mageti kuna mtu amechukua simu za Mheshimiwa Rweikiza zote mbili, kwa hiyo kama una simu ambazo siyo za kwako pia tunaomba tuletee meza kuu

hana ili tuweze kumrudishia mwenyewe. Unajua dunia ya leo mtu akikosa simu tena zote mbili unamchanganya kabisa. Ni bahati mbaya labda mtu amechukua kwa bahati mbaya kwa sababu simu zinafanana.

Naomba niwatangazieni Waheshimiwa Wabunge ambao hamjarejesha fomu zile fomu za manjano, lakini pia fomu za kupangiwa Kamati ambazo mngependa kuhudumia, mkamilishe basi kujaza fomu hizo na kuzikabidhi kwenye dawati la mapokezi lilioko pale jengo la utawala. Mkabidhi zile fomu ili mtupatие mapendekezo yenu na pia mnakumbushwa kukamilisha ujazaji wa fomu za maeleo binafsi kwa matumizi ya ofisi mapema iwezekanavyo. Jamani jazeni zile fomu mtupatие hata huko mbele ya safari zinahitajika zile fomu, mnanisoma? Maana kuna yajayo, sasa hutaeleweka wewe ni nani, ni vizuri ujaze zile fomu zinasaidia saidia kwenye kuchambua chambua, zinamrahishishia Mheshimiwa Waziri Mkuu kukufahamu, Mheshimiwa Rais kukufahamu, Mheshimiwa Makamu wa Rais na Spika kukufahamu pia na wengine wote. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, ni muhimu sana kuzijaza zile fomu na tuzijaze kwa ukweli. Tulipata matatizo siku za nyuma; unajaza jina la mke mwingine baada ya muda mke wa kweli anakuja kwa Spika, mimi mama fulani unamwambia mama wewe humo au kwa akina mama lijazwe jina la baba kweli. Baadae yanaleta shida haya mambo haya, yanaleta mtafaruku hasa rafiki zangu Wasukuma wana matatizo sana, wanajaza Bi mdogo badala ya Bi mkubwa.

Waheshimiwa Wabunge, sasa niwatambulishie kidogo wageni ambao tunao pale *Speaker's Gallery*:-

Mgeni wangu ni Mheshimiwa Balozi Dkt. Batilda Salha Buriani. Mheshimiwa Balozi Buriani aliwahi kuwa Mbunge hapa, tulikuwa naye na alikuwa *Chief Whip* wakati huo, baadaye akaenda kuwa Balozi Nairobi na baadaye akaenda Japan na sasa tuko nae hapa nchini, ni Kada maarufu wa Chama cha Mapinduzi. Safari hii amepambana sana kule Karatu kumleta Mbunge wa Karatu humu ndani,

Mbunge wa Karatu yupo wapi? Yule pale, karibu sana. Mheshimiwa Buriani alikuwa mmojawapo wa wapambanaji kule Karatu. (*Makofi*)

Pia hapo kwenye *gallery* tunae Ndugu Emmanuel Lawrence ambaye ni mdogo wake na Mheshimiwa Buriani. Ahsante, karibu Emmanuel. (*Makofi*)

Vilevile tunao madareva Wanawake Tanzania wakiongozwa na, hawa wote wanatoka umoja wa madereva Wanawake Tanzania. Wapo Naetwa Ihema, yuko Happiness Alloyce, yuko Miriam Mchunga, yupo Judith Mathew na yuko Rehema Chacha. Hawa ni madereva maarufu sana, yaani ni mahiri sana hawa. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge kama hamna madereva...(*Kicheko*)

Tunawapongeza sana kwa kuwa mfano, sijapata maelezo ya kutosha kuhusu shughuli mnazozifanya *exactly* lakini niwapongezeni sana na mnaongoza njia kwa wasichana wengi ambaao wako huko ambaao pia wangeweza kuingia katika kada hii ya udereva wa magari ya aina kwa aina. Kwa hiyo, nawapongeza sana, mwendelee kuwa imara na kwa kweli madereva wanawake ni makini sana barabarani, hata ajali zao ni chache sana na ajali nyingi zinakuwa wao wamegongwa badala ya kugonga. Nawapongeza sana, karibuni sana na mtushauri kama kuna jambo kama Bunge tunaweza tukafanya katika kuboresha hali ya udereva kwa wanawake katika nchi yetu ili muweze kuwa wengi, wengi, wengi kadri iwezekanavyo, karibuni sana. (*Makofi*)

Ndugu Usia Ledama kutoka *UNICEF-Tanzania*, yupo Ledama? Naona atakuwa ametoka kidogo.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wako wageni wa Mheshimiwa Tulia Ackson ambaao ni mume wake James Mwainyekule. James Waheshimiwa hawajakuona bwana usimame tena na hasa kule Mbeya wakuone bwana maana yake wengine walisema hayupo, hayupo. Ahsante sana, jamani Shemeji yetu huyo. (*Makofi/Kicheko/Vigelegele*)

Pia wako Ndugu zake Mheshimiwa Tulia ambaao ni Roima, Beatrice, Royda Ackson wote hawa. Roima, Beatrice na Royda? Karibuni sana hawa ni ndugu za kuzaliwa naye. Ahsante sana na karibuni sana. Vile vile yuko Zena, karibu sana Zena, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia viongozi wa CCM Mbeya wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Mbeya Mjini, Ndugu Alfred Nsomba. Mwenyekiti? Ahsante sana. Wengine Ndugu Ally Majeshi Ally, Philemon Mng'ong'o, James Machaku, Nafueli Mathias na Anitha Majeshi kutoka Mbeya wapo? Mko pale ahsante sana na karibuni sana. Na wapiga kura kutoka kule Mbeya mkiongozwa na Given Tughimbe. Naomba wapiga kura kutoka Mbeya wote tusimame tuliokuja leo. Ahsanteni sana karibuni sana, sana. (*Makofi*)

Naona Mheshimiwa Aida anawakodolea macho anaangalia, anasema iko kazi maana yake yeye kaponea tundu la sindano. Ila Mheshimiwa Aida bwana umetupiga, maana yake Keissy mpiganaji wetu, umeenda kupiga pale pale. huyu Mheshimiwa Aida huyu hatari. Hapo tunakubali Mheshimiwa Aida. (*Kicheko*)

Mgeni wa Mheshimiwa William Lukuvi, Ndugu Naima Malima na Ndugu Warda Obathan. Karibuni sana popote pale mlipo, karibu sana. (*Makofi*)

Wageni sita wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa ambaao wanatoka Karagwe Mkoa wa Kagera wakiongozwa na Ndugu Eliud Rwechungura. Wale kule juu karibuni sana, sana, kutoka Karagwe ni mbali kweli karibuni sana. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambaye ni mpiga kura wake kutoka Mkoa wa Songwe, Ndugu Joanarka Siza. Karibu sana. (*Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Anastazia Wambura ambaye ni familia yake kutoka Mkoa wa Mtwara ndugu Verena Mahundu, ndugu Raphael Amwiru na ndugu Salum Tino. Karibuni sana kutoka Mtwara. (*Makofi*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Bonnah Kamoli ambaao ni Fatuma Lomo na ndugu Jafari Kwembe. Karibuni sana. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Hussein Bashe ambaye ni dada yake ndugu Dalasho Bashe. Dalasho yuko wapi? Dalasho hatujakuona. Jamani ndiyo dada yake Mheshimiwa Bashe, yuko vizuri, mtoto wa Kinyamwezi huyo. Waheshimiwa wanasesma baadaye uwaoneone kidogo, uwepo wepo viwanja vya Bunge. (*Makofi/Kicheko*)

Wageni 17 wa Mheshimiwa Rose Tweve ambaao ni ndugu na rafiki zake kutoka Mafinga Mkao wa Iringa wakiongozwa na Ndugu Sabina Msigwa. Wale wageni kutoka Iringa karibuni sana, sana. Wote 17 karibuni msimame, ahsanteni sana kokote kule mlipo, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni 32 wa Mheshimiwa Waitara Mwita ambaao ni wapiga kura wake kutoka Tarime Vijijini Mkao wa Mara wakiongozwa na Mama yake mzazi ndugu Nyamogesi Mwikwabe. Karibuni sana, sana kutoka Tarime Kanda maalum, karibuni sana. Ahsante, mnawenza kukaa, ila sasa naomba Mama wa Mheshimiwa Mwita Waitara mama mzazi, yuko wapi mama? Ahsante, jamani mnamuona mama? Makofi kwa mama yetu jamani. Ahsante sana mama, ubarikiwe sana, ahsante sana. (*Makofi*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Damas Ndumbaro ambaao ni familia yake kutoka Songea Mkao wa Ruvuma wakiongozwa na ndugu Flora Ndumbaro. Karibuni sana, wale pale ahsante sana, karibuni sana. Dada Flora yuko wapi? Flora huyo, maua hayo, ahsante. (*Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Philip Mulugo ambaao ni Katibu Mwenezi Mkao wa Songwe Ndugu John Zumba, Katibu wa CCM Wilaya ya Momba ndugu Omar Ng'wamang'wali na Katibu ya Jumuiya ya Wazazi ndugu Nicholaus Chibwana. Karibu sana wale kutoka Songwe. (*Makofi*)

Wageni 10 wa Mheshimiwa Ndaisaba Ruhoro kutoka Mkoa wa Ngara Kagera wakiongozwa na Ndugu Deogratius Manyaga. Karibuni sana. (*Makofii*)

Mwisho ni wageni watatu wa Mheshimiwa Masache Kasaka kutoka Lupa, ndugu Flora Horonga Kasaka na ndugu Masache Kasaka na ndugu Fadhili Maures. Karibuni sana, wale wa kutoka kule Lupa. (*Makofii*)

Uongozi wa Benki ya *DCB* kule *gallery* naomba msimame. Karibuni sana akiwepo *DG* wa Benki ya *DCB* hii ni Benki mojawapo zenye Matawi ambazo ziko hapa Mjini Waheshimiwa Wabunge na wana banda lao watakuwa nalo hapa tuwatembelee ili tuweze kujifunza *facilities* ambazo wanazitoa ambazo ni *very competitive*.

Pia tunao uongozi wa *NMB* kutoka Makao Makuu ya Benki ya *NMB* karibuni sana *NMB* na wapendwa wetu pia na wana *packages* zao pia nzuri safari hii basi msisahau kuwatembelea pia *NMB*. (*Makofii*)

Sasa Waheshimiwa Wabunge tayari ninayo matokeo ya kura zilizopigwa. Idadi ya kura zilizopigwa jumla zote ni 350, hakuna kura yoyote iliyoharibika. Kura ya hapana hakuna hata moja, zote 350 zimemthibitisha Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa amethibitsihwa na Bunge hili kuwa Waziri Mkuu kamili kwa jumla ya kura 350 za ndiyo sawa na asilimia mia moja. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. Ni upendo wa hali ya juu sana na ni imani ya hali ya juu sana, nawashukuruni sana, sana. (*Makofii/Vigelegele*)

Sasa wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anajiandaa kuja kuzngumza nasi, nimalizie utambulisho kwa kuwatambulisha wageni kama 50 hivi kutoka Kisesa kwenye Jimbo la Mheshimiwa Mpina. Wale wageni wa kutoka kwa Mpina karibuni msimame, karibuni sana, sana hapa Dodoma. Karibuni sana Wasukuma wangu, mijisikie mko nyumbani. Basi mnawenza mkakaa, muwe makini huko barabarani msije

mkagongwa na magari, maana yake Wasukuma ninyi washamba washamba hivi. (*Makofi/Kicheko*)

Kipekee niwasimamishe wazazi wa Mheshimiwa Mpina, Baba na Mama wa Mheshimiwa Mpina naomba msimame. Ahsante sana, ahsante sana Baba, ahsante Mayo, ahsanteni sana jamani ndiyo wazazi wa Mheshimiwa mwenzetu. Ahsante sana na mbarikiwe sana kwa kusafiri kutoka mbali kuja kututembelea na katuona. (*Makofi*)

Basi baada ya matangazo ya wageni hao, basi Mheshimiwa Waziri Mkuu tukupatie nafasi, uje hapa mbele kama una neno la kuzungumza nasi, karibu sana. (*Makofi*)

MHE. KASSIM M. MAJALIWA - WAZIRI MKUU MTEULE:
Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameendelea kutupa uhai sisi sote na hasa Waheshimiwa Wabunge amba tuko hapa pamoja na mimi pia kuwepo hapa mbele ya Bunge lako Tukufu na kushuhudia, haya yote ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kwa dhati yangu ya moyo nimshukuru sana Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini kabla sijaanza kumshukuru nimpongeze sana yeye mwenyewe kwa ushindi mkubwa alioupata kutoka kwa Watanzania kuititia uchaguzi tulio umaliza siku chache zilizopita amba ameshinda kwa kishindo wenye imani kubwa ya Watanzania kuititia uchaguzi uliofanyika kwa uhuru na haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuititia ushindi huu amba pia Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli alikuwa pamoja na Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kama mgombea mwenza na yeye nimpongeze sana kwa ushindi mkubwa amba ameupata kuititia uchaguzi huu. Baada ya kumpongeza kwa ushindi wake mkubwa ambapo nilikuwa sijapata fursa ya kumpongeza hadharani. Kwa kweli nimeona nitumie nafasi hii nimpongeze sana pia kwa uchaguzi huu na

namna ambavyo Watanzania wameridhishwa na kazi kubwa aliyoifanya katika kipindi cha miaka mitano na imani walijonayo kwa kipindi cha miaka mitano mingine kwamba nchi hii itakuwa imefikia hatua nzuri sana, hongera sana Mheshimiwa Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nimeona nitumie nafasi hii nimpongeze sana pia kwa uchaguzi huu na namna ambavyo watanzania wameridhishwa na kazi kubwa aliyoifanya katika kipindi cha miaka mitano na imani walijonayo kwa kipindi cha miaka mitano mingine kwamba nchi hii itakuwa imefikia hatua nzuri sana, ahsante sana, hongera sana Mheshimiwa Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nije sasa kwenye shukrani, jambo hili si dogo najua Mwenyezi Mungu ameliongoza, namshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, kwa imani yake kubwa aliyonayo juu yangu, na kuendelea kuniamini kwamba naweza kufanya hayo niliyoyafanya katika kipindi cha miaka mitano au na zaidi katika kipindi kingine kijacho cha miaka mitano, namshukuru sana Mheshimiwa Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, natambua Mheshimiwa Rais kwa mamlaka yake anapofanya maamuzi haya anaweza pia kumshirikisha Makamu wa Rais, na kwa kuwa wanafanya kazi pamoja, nitumie nafasi hiyo pia kumshukuru mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Makamu wa Rais kwa ushiriki wake katika ridhia jina langu liweze kuja tena mbele ya Bunge Iako Tukufu ili kuomba ridhaa kwa Wabunge wenzangu liweze kuungwa mkono hatimaye niweze kushiriki tena katika shughuli za kuliletea taifa hili maendeleo. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais, namshukuru pia Makamu wa Rais kwa namna yoyote ambayo ameshikiri. (*Makofi/Vigelegiele*)

Mheshimiwa Spika, kwenye hili la shukrani, sina uhakika kama neno hili linatosha, lakini Mwenyezi Mungu anaweza kumpelekea namna ambavyo nahisi moyoni mwangu mimi, mke wangu na watoto wangu na familia yangu, pia wapiga

kura wangu wa Ruangwa ambavyo tunamshukuru Rais kwa kutambua mchango wetu katika kumletea niendelea, katika kumsaidia kufanya kazi. Niendelee kumuhamakishia kwamba matamanio yake yaliyompelekea kutoa jina hili kulileta tena mbele ya Bunge hili Tukufu, matamanio yake ambayo anaamini Wabunge wenzangu na kwa namna ambavyo mmepiga kura nyingi hapa hiyo ni imani tosha kwamba Mheshimiwa Rais ameleta jina ambalo na nyie pia mmnaamini kwamba tutamsaidia kazi. Naomba niwahakikishie nitafanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, najua nitapata nafasi pia ya kukutananae nitamshukuru zaidi nitakapokutananane, lakini leo kwa kweli namshukuru sana na Mwenyezi Mungu aendeleee kumuongezea afya, uwezo, busara, ili aendeleee kulitumikia Taifa hili kwa weledi mkubwa kama msaidizi wake nitamsaidia kadri Mungu atakavyoniwezesha katika kufanya kazi hii. Ahsante sana Mheshimiwa Rais popote ulipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kukushukuru wewe, lakini kabla sijakushukuru, nikupongeze sana kwa ushindi mkubwa uliopata kule kwenye Jimbo letu la Kongwa. Kwa wana Kongwa kukupigia kura nyingi za ndiyo na hatimaye kuwa Mbunge wa Jimbo la Kongwa sambamba na pongezi hizi nikupongeze tena pia kwa kurudi tena kwenye nafasi yako ya Uspika, nafasi iliyotokana na kura za Wabunge kura nyingi za kutosha, kura zilizoonyesha imani nawe kwamba unatosha kuendelea kuwa Spika katika kipindi cha miaka mitano mingine, nawashukuru sana, nakupongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika hili hakuna siri kwamba umefanya kazi mzuri sana miaka mitano iliyopitia kama Spika wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Umeisaidia sana Serikari katika kushauri na kuismamia Serikali kupitia chombo chako hiki cha Bunge lako Tukufu na kuwezesha Serikali kufanya mambo mazuri, makubwa katika nchi na hayo yote yalitokana na mchango wako, hongera sana. Kwa hiyo tunayo imani kwamba kazi uliyoifanya miaka mitano iliyopita utaweza kuifanya kazi hiyo vilevile au zaidi

katika kipindi cha miaka mitano ijayo na tunatarajia tutapata mafanikio makubwa kupitia Serikali kwa kusimamia na kutushauri, na nikuhakikishie kwamba Serikali itaendelea kukupa ushirikiano wa dhati kwa ushauri utakaotolewa na Bunge lako kwa usimamizi utakaoutoa na kwa kuwa nilikuwa Waziri Mkuu katika kipindi kiliochopita kwa kweli naomba nionyeshe faraja yangu kwamba hata haya maamuzi yanayoendelea sasa mchango wako ni mkubwa sana katika kipindi chako cha miaka mitano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niendelee kushukuru kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwa kweli mmenifanyia jambo kubwa sana kwangu na familia yangu. Idadi ya kura zenu, mmenipa changamoto kubwa sana, nimefarijika na nawashukuru sana, changamoto yangu ni kwamba wale wachache ambao tulikuwa kipindi cha miaka mitano iliyopita na wengi mmepata nafasi ya kusema neno na mmeweza pia kuhabarisha Wabunge wapya kwamba tuliweza kufanya kazi pamoja, vizuri na kwa mafanikio makubwa na mmeweza kuwashawishi Wabunge wapya kwamba tunaweza kufanya makubwa zaidi katika kipindi kijacho na hatimaye mmeweza kupiga kura kwa asilimia 100 haijawahi kutokea, nawashukuru sana Wabunge wenzangu. Nawashukuru hivi kwa sababu najua pia tunao Wabunge wa kutoka vyama rafiki vyama vya Upinzani kura asilimia 100 maana yake nawa pia wamepiga kura ya ndiyo waklonyesha imani kubwa kwangu kwa namna ambavyo tutashirikiana katika kipindi hiki cha miaka mitano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie tena kuwahakikishia Wabunge wezangu kwamba nitaendelea kushirikiana na Wabunge wenzangu wote wa Chama Tawala na vyama rafiki, nikijua nyie ni wawakilishi wa watanzania huko waliko kwenye Majimbo yenu wanaotamani kupata maendelea kutokana na uwakilishi wenu. Nataka niwaahidi nitapita tena kwenye maeneo yenu yote, kupata fursa ya kuona shughuli za maendeleo ambazo Wabunge wenzangu mnazisimamia nyie ndiyo mkiwa Wenyelevi wa ushauri wa maendeleo kwenye Wilaya zenu kwenye Majimbo yenu tutapita kwenye Majimbo yenu kukagua miradi mbalimbali,

pia kupata fursa ya kukutana na wananchi wetu, kuwasikiliza na kuona namna ya kupokea kero zao na namna mzuri ya kutatua kero zao. Na nitafanya hilo kwa Majimbo yote ya wana CCM kwa Majimbo yote ya ndugu zetu wa vyama rafiki, tukijua kwamba walioko huko ni watanzania wa vyama vyote na maendeleo bado kauli yetu hayana chama, maendeleo ni ya watanzania wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutembelea kwenye Majimbo yote niwahakikishie kuwapa ushirikiana wa hapa ndani ya Bunge, na kwa nafasi yangu ambayo baadaye itahitimiswa na kukamilisha taratibu zote, ni kupokea ushauri wenu, kupata ushauri kutoka maeneo mbalimbali. Niwahakikishie nitaendelea kupokea ushauri wenu, nitaendelea kusikiliza yale ambayo mmeyaleta kutoka kwenye Majimbo yetu, changamoto zetu na kuziwekeea utaratibu wa namna ya kwenda kutatua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kijacho, Mheshimiwa Rais ataunda Baraza lake la Mawaziri, na nitakuwa nao hapa ndani, niwahakikishie wote watakaopata uteuzi wa nafasi ya Uwaziri, Naibu Waziri wakiwa hapa ndani wakiwa ni sehemu ya Serikali niwaahidi kwa niaba yao ingawa bado hawajachaguliwa kwamba tutawatumikia Wabunge wote, ili malengo ya Serikali, Serikali iliyoundwa cha Chama cha Mapinduzi chama kilichotengeneza ilani mzuri iliyosheheni maendeleo, maendeleo hayo yaweze kuwafikia watanzania popote walipo. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge wenzangu niwahakikishie tutafanya kazi pamoja tutaendelea kushirikiana ili tufikie hatua ile mzuri tunayoitarajia na ambayo pia imewekewa kama malengo kuititia ilani ya Chama cha Mapinduzi chama ambacho kimeunda Serikali ambayo sasa inaendelea kuimariswa kwenye nafasi zake zote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikiwa nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba tutaaendelea kushirikiana pamoja, niishukuru sana familia yangu mke wangu na watoto wangu ambao wakati wote katika kipindi kilichopita wamenipa ushirikiano mzuri sana wakati wote nilipokuwa nafanya kazi za Serikali, wamenivumilia sana

wakati mwingine wamebaki peke yao, lakini wamebaki kwa faraja kwamba nafanya kazi nikiwatumikia watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, na ninayo imani na wanaungana na mimi kwa shukrani kwa wote ambao nimewashukuru na naamini ahadi yao kuendelea kunipa nafasi ya kufanya kazi na watanzania. Kwa hiyo naishukuru sana familia yangu hii kwa kunipa moyo, kunitia moyo wakati mwingine na kunitia imani katika kufanya kazi za watanzania. Nataka niwahakikishie kwamba familia yangu iko tayari pia ya kuendelea kunipa fursa ya kuwatumikia watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ninapoishukuru familia siwezi kuwasahau pia wapiga kura wangu wa Jimbo la Ruangwa si tu wana Ruangwa hata wana Mkoa wa Lindi, nilmeona nilipopita wakiahidi kupiga kura nyingi sana kwa Chama cha Mapinduzi kwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wamefanya hivyo. Kwa hiyo, niwashukuru sana wapiga kura wa Jimbo la Ruangwa, nawashukuru sana wazee wangu, mama zangu na vijana wote wa Jimbo la Ruangwa kwa kunipa muda mwingi kipindi cha miaka mitano kulitumikia Taifa hili na kukubali muda mfupi wa kwenda Ruangwa kushirikiana nao katika kuleta maendele na sasa Wabunge wameridhia ombi la Mheshimiwa Rais niendelee tena, bado niwahakikishie wana Ruangwa kwa utaratibu ule ule nitaendelea kuwatumikia watanzania kwa kupita maeneo yao yote na muda mwingi kushughulika na habari za watanzania, pia sitawasahau wana Ruangwa katika kufikia malengo letu ya kupata maendeleo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, imani mlionyesha kipindi cha miaka mitano iliyopita naamini imani hiyo hiyo mtaionyesha na mtanipa fursa ya kuwatumikia watanzania miaka mitano ijayo. Nawashukuru sana na nirudie tena kwamba wana Ruangwa sitawaangusha tutafanya kazi za maendeleo ndani ya Wilaya ya Ruangwa, lakini tutafanya kazi za maendeleo kwa watanzania wengine kote nchini, ahsante sana wana Ruangwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa uchache kama ulivyosema basi nikishukuru sana chama changu cha Mapinduzi. Chama cha Mapinduzi kilichokwu kimeridhia kuwa mgombea wa Jimbo la Ruangwa na wana Ruangwa wakasema hatuna sababu ya kukuambatanisha na mgombea mwингine wa Chama Cha Mapinduzi, nikapita bila kupingwa kwenye mchakato wa ndani ya chama, na mchakato huo ulienda pia hata kwa ngazi ya Wilaya hakukuwa na vyama rafiki ambavyo viliamua kuweka mgombea wakanipitisha bial kupingwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii ni imani ya wana Ruangwa pia kwa Chama cha Mapinduzi kwa kuwa maendeleo tunayoleta Ruangwa ni ya wote bila kujali chama na kwenye Chama cha Mapinduzi kwa uongozi wake na usimamizi wake pale Wilayani Ruangwa nawashukuru sana na naamini wataendelea kufanya kazi hata nikiwa siro na ndiyo hao ambaao pia wameendelea kushikiana nami wakati wote nikiwa huku, pia chama Makao Makuu kuititia vikao vyote vyta juu kuridhia kuitisha jina langu kuwa mgombea, pia kuridhia kuwa msimamizi wa ilani ya uchaguzi kwa nafasi ya Uwaziri Mkuu maana yake nayo pia ni ridhaa ya Chama cha Mapinduzi, pia kunipa fursa ya kunipa nchi nzima napita naeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi na matarajio ya ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa watanzania wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haya yote haya siwezi kuondoka hapa bila kukishukuru chama changu Chama cha Mapinduzi. Ni imani yangu chama chetu tutaendelea kusimamia utekelezaji wa ilani ile, na watanzania wote mnajua ilani yetu ya mwaka 2020/2025 ni ilani iliyosheheni maendelea na iliyojazwa kwenye kumbukumbu yenye kurasa zaidi ya 303. Ilani hii kama ambavyo tumeleza na tumeahidi nataka nirudie tena na Mheshimiwa Rais wetu ameeleza kwamba tutaitekeleza kwa zaidi ya asilimia 90. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilazimika pia nikishukuru chama changu cha Mapinduzi ndicho ambacho leo hii kimeunda Serikali, inaongozwa na Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli ambaye ndiyo Mwenyekiti wetu na Rais huyu ndiyo

ambaye ameleta jina hapa kuomba ridhaa kwa Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Wabunge mmeweza kuridhia, haya yote ni mwenendo wa matamanio ya Chama cha Mapinduzi katika kutufikia malengo ambayo tumeyaweka kwa ajili ya utekelezaji wa ilani hiyo kwa watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa nishukuru viongozi na watumishi wa Bunge letu Tukufu, wakiongozwa na mtendaji wetu Mkuu ambaye ni Katibu wa Bunge Mheshimiwa Kagaigai ambaye pia yupo hapa mbele yetu, Bunge hili na kupitia watumishi hawa wamefanya kazi kubwa sana ya kutusaidia sisi Wabunge mwenyewe nikiwemo kwa majukumu yangu ya Kibunge nikiwa hapa Bungeni katika kuipindi cha miaka mitano na ninaimani wataendelea pia kutusaidia kutuongoza, kutuelekeza, kutuhudumia katika kipindi cha miaka mitano ijayo. Nawashukuru sana watumishi wa Wabunge wakiongozwa na Katibu wetu wa Bunge na bado tuna imani kubwa na Bunge letu Bunge lenye hadhi, lenye heshima Bunge ambalo linatenda vizuri na lina sifa chungu mzima ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwamba ni Bunge ambalo lina viwango vya kutosha kuweza kusimamia Bunge letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa imani hiyo na shukrani hizo na pongezi hizo kama ulivyosema niseme machache na kwa kweli leo sina jambo kubwa, tukio la leo hili limenipa mshtuko, pia faraja ya kupita kiasi sikutarajia tulikuwa hapa sote kabla hakuna ambaye alikuwa ana uhakika na hili jambo. Kwa hiyo liliopokuja kwa kweli limetushtua. Kwa hiyo na mimi niendelee kushukuru kwa namna yoyote. Pamoja na utumishi wangu kipindi hiki cha miaka mitano iliopita, lakini mnakumbuka Mheshimiwa Rais katika nyakati kadhaa anasema kwenye Baraza la Mawaziri huku lazima nitashughulika nalo. Kwa hiyo, nilikuwa ni mmoja kati ya Wajumbe wa Baraza la Mawaziri, kwa hiyo hakuna ambaye alikuwa anauhakika. Kwa hiyo, jambo hili nimelipokea kwa mikono miwili namshukuru Mwenyezi Mungu, namshukuru Rais, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwa kuridhia,

nashukuru chama changu na wote ambao wana mapenzi mema katika utekelezaji wa shughuli zetu za Serikali.

Baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa kuridhia kunipa muda huu kusema haya niliyosema, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Sasa Mheshimiwa *PM* tukuombe sasa, tukuombe uende kwenye kiti chako sasa Mheshimiwa utuachie hiki cha kwetu sasa, ahsante sana Waheshimiwa Wabunge. Sasa wote tunapumua. (*Kicheko/Vigelegele*)

Kwa heshima ya Wabunge wageni, kiti cha Mheshimiwa Waziri mkuu ndiyo hicho na kile kiti cha kwanza mkono wa kulia huwa kiko wazi muda wote. Huwa kiko wazi kwa sababu, inawezekana jimboni huko una jambo kubwa limetokea ambalo unadhani ni vizuri ukamwasilishia Mheshimiwa Waziri Mkuu moja kwa moja badala ya kulileta hapa, basi kiti kile huwa ni kwa ajili yetu. Sasa wakati shughuli za Bunge zinapoendelea, basi uwe na jambo kweli la maana, siyo unakwenda kupiga michapo pale, itakuwa tena unawazuia Wabunge wanaosema humu ndani ambao inabidi yeye awasikie, wasiweze kufikisha ujumbe wao moja kwa moja.

Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa niaba ya Wabunge wote, nami napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza sana sana sana kwa uteuzi huu. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuturudishia wewe. Tumefanya kazi pamoja kwa miaka mitano, tayari tunafahamiana. Nina hakika kabisa ushirikiano wetu utakuwa mkubwa zaidi huko tunakoenda na hali ya utulivu Bungeni itakuwa kubwa zaidi, kwa sababu kwa kweli, Bunge ndiyo mahali ambapo siasa zinahamia kwa miaka mitano. Zinatoka mitaani tulikotoka kwenye kampeni, sasa zinahamia hapa. Kwa hiyo, hata kama hapa asilimia kubwa ni Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, kawaida ya wanasi sasa wanapokutana, shughuli iko pale pale.

Kwa hiyo, tunakutegemea sana mwenzetu kama kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni, nasi Wabunge wote

tutakuwa na ushirikiano. Ila tuna hakika kuitia wewe mwenzetu mambo ya Waheshimiwa Wabunge yatafika Serikalini, kama ulivyoahidi bila ubaguzi wa aina yoyote. Serikali yetu ni sikivu, basi kuitia wewe wananchi wetu watafaidika na kunufaika.

Tunashukuru sana, tunakutakia kila la heri. Ahadi yetu kwako ni kukupa kila aina ya ushirikiano. Ahsante sana. (*Makofii*)

Sasa Waheshimiwa Wabunge shughuli za leo lazima zikamiliike. Naitazama saa yangu hapa, lakini iwe iwavyo lazima tumalize shughuli hizi leo, kwa maana ya kumpata Naibu Spika, ili baada ya hapo, sasa tuahirishe shughuli hadi kesho kwa ajili ya lile jambo kubwa ambapo Mheshimiwa Rais atatuhutubia kwa maana ya kuzindua rasmi Bunge hili la Kumi na Mbili.

Katibu, sasa tuendelee.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

UCHAGUZI WA NAIBU SPIKA

SPIKA: Maelezo kutoka kwa Katibu.

MAELEZO YA KATIBU WA BUNGE KUHUSU UCHAGUZI WA NAIBU SPIKA

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

Mheshimiwa Spika, kama orodha ya shughuli za leo inavyoonesha, kutakuwa na uchaguzi wa Naibu Spika unaofanyika kwa mujibu wa Ibara ya 86(2) na (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 pamoja na Kanuni ya 11 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 86(2) ya Katiba inaelekeza kuwa Uchaguzi wa Naibu Spika utafanyika wakati wowote katika Mkutano wa Kwanza wa Bunge jipya au katika

kikao cha kwanza cha Bunge mara baada ya kutokea nafasi katika kitu cha Naibu Spika. Aidha, kwa mujibu wa Ibara ya 85(1) ya Katiba na Kanuni 11(3), Naibu Spika huchaguliwa kutoka mionganini mwa Wabunge na uchaguzi huo hufanyika baada ya Wabunge kuapa kiapo cha uaminifu.

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi masharti ya Katiba niliyoyaainisha hapa juu, tarehe 5 Novemba, 2020 nilitoa Tangazo Namba 1764A katika Gazeti la Serikali, Toleo Maalum kutangaza kuwa Uchaguzi wa Naibu Spika utafanyika tarehe 12 Novemba mwaka huu na utaratibu utakaotumika kwenye uchaguzi huo.

Aidha, nilielekeza kwamba, chama chochote cha siasa chenye uwakilishi Bungeni kinachokusudia kushiriki katika uchaguzi wa Naibu Spika wa Bunge kiwasilishe jina la mgombea wa chama husika Ofisiini kwa Katibu wa Bunge, Dodoma kabla ya saa 10.00 jioni tarehe 11 Novemba, ambayo ndio siku ya uteuzi.

Mheshimiwa Spika, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi kufikia saa 10.00 jioni ya tarehe 11 Novemba, mwaka huu 2020 nilikuwa nimepokea jina la mgombea mmoja tu ambaye ni Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kutoka Chama cha Mapinduzi. Kwa kuwa, tunaye mgombea mmoja tu, utaratibu utakaofuatwa ni kwamba mgombea huyo atafika mbele yenu ili kujieleza kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza, kuulizwa na kujibu maswali kama yatakuwepo na kisha kuomba kura.

Mheshimiwa Spika, baada ya zoezi hilo kukamilika, kila Mbunge atapewa karatasi ya kura yenye jina la mgombea na atatakiwa kupiga kura ya "Ndiyo" au "Hapana" mbele ya jina hilo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kura zitakuwa za siri ambapo kila Mbunge atapiga kura yake mahali alipoketi na baada ya hapo masanduku ya kura yataletwa hapa yakiwa wazi ili ninyi Waheshimiwa Wabunge kama wapiga kura muweze kuyathibitisha.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 7(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 iwapo mgombea huyo atapata kura nyingi za "Ndiyo" atatangazwa kuwa amechaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, naomba sasa tuendelee na zoezi la mgombea kujieleza na kupiga kura.

SPIKA: Ahsante sana katibu kwa maelezo hayo.

Waheshimiwa Wabunge, tunazidi kujifunza namna na *sequence* ya mambo yanavyoenda katika Bunge. Mtaona kwamba Spika, huwa anawenza kupatikana mionganoni mwa Wabunge au mionganoni mwa wananchi wenyewe sifa za kuwa Wabunge, lakini wasiokuwa Wabunge. Ndiyo maana utaratibu wake ni ule tuliofuata katika kumpata Spika.

Pia mtaona kwamba, tunampata Naibu Spika; kwanza Naibu Spika huwa ni lazima awe Mbunge tofauti na Spika. Unaweza ukawa na Spika sio Mbunge, unaweza ukawa na Spika ambaye ni Spika, lakini pia ni Mbunge kama nilivyo mimi. Ila Naibu Spika ni lazima awe Mbunge; na hii ni *CommonWealth Practice Kwamba assuming Spika sio Mbunge, lazima katika uongozi wa Bunge pawe na mtu ambaye anatokana na Wabunge ili kuendana pamoja.*

Kwa hiyo, ndiyo maana lazima Naibu Spika atokane na Waheshimiwa Wabunge na anakuja baada ya uchaguzi wa Waziri Mkuu kwa sababu naye anakuwa kwenye *pool* nyingine yoyote. Nafikiri mnanielewa. Naye anakuwa kwenye *pool*/kama tulivyokuwa kwenye *pool/sisi* wote wakati ule, lakini sasa baada ya kumpata Mheshimiwa Waziri Mkuu sasa tunaendelea na *structures* nyingine zote.

Kwa hiyo, sasa ni wakati wa uchaguzi wa kuweza kumpata msaidizi wangu mkuu. Pendekezo hapa ni la ndugu yetu, mwenzetu, mionganoni mwetu, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu, ambaye nitamwomba sasa aweze

kuingia hapa na aweze kutoa maelezo kidogo ya kuomba kura.

Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson. (*Makof*)

(*Mhe. Dkt. Tulia Ackson - mgombea nafasi ya Naibu Spika, alisogea mbele kwa ajilli ya kujieleza na kuomba kura*)

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, mbele yako ni wapiga kura, mbele yako ni Wajumbe... (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, nilichokisema wala sijakosea. Ndiyo maana majina yenu yote mnaandikwa Mheshimiwa fulani, fulani, mbele yake linawekwa neno Mb., si mnaona eeh? Lile neno Mb. huwa ni nini? (*Kicheko*)

MBUNGE FULANI: Mbunge!

SPIKA: Mmekosa, lile neno Mb. huwa ni Mjumbe wa Bunge, kufuatana na Katiba. Kwa hiyo, Wabunge ni Wajumbe; na wajumbe ni noma. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Dkt. Tulia karibu sana uongee na Waheshimiwa Wabunge.

MHE. DKT. TULIA ACKSON: Mheshimiwa Spika, Job Yustino Ndugai, ambaye ni Spika wetu wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha sisi sote kuwa hapa, lakini nami kunisimamisha hapa mbele yenu Wabunge ili niweze kuokmba fursa kwenu na kwa wananchi wote ya kumsaidia Mheshimiwa Spika kazi ya kuliongoza Bunge. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na fursa hii ya kuomba kura kwenu, lakini Mheshimiwa Spika naomba uniruhusu kwa

sababu wako viongozi ambao wameshapatikana kabla yangu, niwapongeze. Nianze na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano a Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa ushindi mkubwa sana aliouputa. Ninampongeza sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pamoja naye nimpongeze mama yetu, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kumsaidiu Mheshimiwa Rais na wananchi wamewaamini wote pamoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ametoka hapa muda siyo mrefu. Ninampongeza kwa kupata kura asilimia 100, na pia kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais, nasi Wabunge tukakubaliana na hilo. Hongera sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nawe ulipitia mchakato huu, umetutangulia sisi wengine. Nachukua fursa hii kukupongeza sana sana kwa ushindi mkubwa uliouputa na Wabunge hawa wakakuamini nami nikiwa mmoja wao. Nakupongeza sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kwa ushindi mkubwa aliouputa; ambaye alikuwa Mbunge mwenzetu, lakini sasa ye ye amepata fursa ya kuwa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, tunakupongeza sana. (*Makof*)

Ndugu zangu nawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge wote. Amesema Mheshimiwa Spika hapa mambo ya Wajumbe, lakini mambo yalienda vizuri. Ninawapongeza sana sana kwa ushindi mkubwa mliouputa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu baada ya pongezi hizo, nitoe shukrani za kipekee sana kwa kila mmoja aliyeusika kunifikisha hapa. Kwa sababu, leo ni siku ya kuomba kura, sitaweza kumtaja kila mmoja ama kila kundi

ambalo limesaidia mimi kufika hapa, lakini kila mmoja kwa mchango wake mkubwa ambao umenifikasiha hapa siku ya leo, ninamshukuru sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee kabisa sisi sote ambao tunahusika katika mimi kusimama hapa mniruhusu nitaje makundi matatu. Kwanza ni Chama cha Mapinduzi ambacho kinaongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, ambaye nilipata fursa ya kuaminiwa naye kwa sababu pengine nisingesimama hapa kama ye ye asingeniibua na kuingia kwenye siasa. Kwa hiyo, kwa namna ya kipekee sana ye ye kama Mwenyekiti wetu wa Chama ninamshukuru sana sana pamoja na viongozi wengine. Ninavyomtaja ye ye, ni ngazi zote za Chama mpaka kuwafikia Wajumbe ambao walipiga kura kule Mbeya Mjini. Ninawashukuru. Wengine wako hapa leo kushuhudia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukrani hizo kwa Chama changu cha Mapinduzi, pia nawashukuru sana sana wapiga kura wa Mbeya Mjini kwa heshima kubwa sana ambayo wamenipa ya kuwa humu ndani siku ya leo. Kama mnavyofahamu, ili niweze kugombea nafasi hii, ni lazima niwe Mbunge. Kwa hiyo, wao wameniwezesha pia kusimamama hapa na kwa namna ya kipekee ninawashukuru sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia ninaishukuru familia yangu kwa ujumla, ahsanteni sana kwa kuwa pamoja nami wakati wote. Ninawashukuru sana. Ndugu zangu muda wangu ni mfupi, shukrani hizi zitoshe kwenu nyote ambao mnahusika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nije mbele yenu Waheshimiwa Wabunge kuwaomba fursa ya kuwa Naibu Spika, kwa maana ya Msaidizi Mkuu wa Spika wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwenye Bunge la Kumi na Moja Mheshimiwa Ndugai alikuwa Spika, nami nilimsaidia. Tulijitahidi kadiri tulivyowenza kuisimamia, kuishauri Serikali na pia kwa kushirkiana na Wabunge kufanya yote yale ambayo sitaki kuyarejea, ameyaeleza kwa kirefu Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Tulijitahidi kufanya hivyo na tunatamani tuendelee kufanya hivyo. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, naomba kura zenu ili niweze kuwa Msaidizi Mkuu wa Mheshimiwa Spika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu nawe ni mpiga kura na hapa nimetaja Wabunge, pamoja na kwamba na wewe ni Mbunge, nawe naomba kura yako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nimalizie kwa kusema Waheshimiwa Wabunge naombeni sana kura zenu.

Mheshimiwa Spika, ahsanteni kwa kuniskiliza. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana mgombea. Kama ilivyo ada, kama kuna swali lolote! Maswali! Swali lipo. Nimekuona Mheshimiwa Aida Khenan, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, tafadhali uliza swali lako. (*Kicheko*)

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Napenda kuuliza swali moja kwa dada yangu, Mheshimiwa Tulia Ackson, Mbunge wa Mbeya Mjini.

Mheshimiwa Spika, sina mashaka na uzoefu wa mgombea kwenye nafasi anayoliomba. Natambua kwamba nafasi hiyo ndiyo aliyokuwanyo kwenye Bunge lillopita. (*Makofii*)

Mheshimiwa mgombea, mionganini mwa changamoto ambazo zilikuwepo Bunge lillopita ni pamoja na changamoto ya muda kwa Wabunge kuchangia ndani ya Bunge, jambo ambalo kwa wananchi pia ilikuwa ni changamoto kidogo. Ningependa kujua umejipangaje juu ya kuweza kuwapa nafasi au muda wa kutosha Wabunge ili waweze kuwakilisha mawazo ya wananchi waliowaamini bila kuathiri kanuni?

SPIKA: Bado nafikiria, natafakari, hili ni swali au siyo swali?

Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, majibu tafadhalii.

MHE. DKT. TULIA ACKSON: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa fursa hii ya kujibu swali hili ambalo nimeulizwa na mjumbe, Mheshimiwa Mbunge wa Nkasi Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, mimi kama msaidizi wako mkuu, ni wajibu wangu kukushauri katika yale mambo ambayo yatanipata kutoka kwa Wabunge, kwa maana ya hoja zao za mambo wanayotaka yabadilike. Kwa jibu la moja kwa moja ni kwamba, muda tumeuweka sisi wenyewe Waheshimiwa Wabunge kwenye kanuni ambazo tunao uwezo wa kuzibadili muda wowote tukiona inafaa.

Kwa muktadha huo, maadam umelisema leo, nami naomba nafasi ya kuwa msaidizi wa Mheshimiwa Spika basi nikiipata hiyo nafasi tutapata fursa ya kulitazama hili jambo kwa mapana zaidi na kuona namna bora ya kuendesha Bunge ili Wabunge waweze kupata fursa ya kuwawakilisha wananchi wao kwa muda unaowatosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Swali la pili kama lipo. Ndiyo nimeona, Mheshimiwa nimkuona tafadhalii.

MHE. VUMA A. HOLLE: Mheshimiwa Mgombea, kwanza nikupongeze kwa kazi ambayo umeifanya kwa miaka mitano. Nina swali moja dogo tu. Bunge hili tunaona ni Bunge ambalo idadi ya vijana imeongezeka. Sasa wewe kama Msaidizi Mkuu wa Spika unatuahidi nini sisi Wabunge vijana ili kuhakikisha kwamba, uwakilishi wetu hapa unastawi na tunatimiza majukumu yetu vizuri ili Bunge ijalo tuweze kuongezeka wengi zaidi?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Tulia Ackson, majibu ya swali hilo, Wabunge vijana.

MHE. DKT. TULIA ACKSON: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa ya kujibu swali liloulizwa na Mheshimiwa Vuma. Bunge lako linayo makundi mbalimbali, wengine ni wawakilishi wa makundi, lakini wengine wako kwenye hayo makundi mbalimbali, lakini ni wa rika mbalimbali, lakini pia jinsia tofauti. Makundi yote hayo ni wajibu wangu kama msaidizi wako kuyahudumia na kuhakikisha wanawakilisha wale wananchi ambao wamewatuma vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni wazi kundi la vijana ni kubwa na mimi kama mwenye umri wa kati hivi nitakutana nao bila shaka, wasiwe na wasiwasi. Watapata ushauri wa kutosha ili vijana hawa waweze kuwa wawakilishi wazuri lakini pia waweze kukaa humu ndani kama ambavyo amekaa Mheshimiwa Lukuvi. Wakishanipa kura, ukinipa hilo jukumu mimi nitawalea hawa vijana kwa hiyo wasiwe na wasiwasi. (*Makofi*)

SPIKA: Swali la tatu na la mwisho, kuna mkono; ndiyo.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kumuuliza mgombea Unaibu Spika swali la tatu na la mwisho.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa mgombea wa Unaibu Spika, tumekuwa wote katika Bunge lililopita lakini wewe mwenyewe ni shahidi, umeshuhudia matatizo mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge, hasa wanapokuwa nje ya Bunge lako Tukufu, hasa barabarani kunyanyasika, kukamatwa na kutaka kujieleza maneno mengi. Sasa wewe kama Naibu Spika, tumekuwa tukilalamika sana kwa Mawaziri hapa na pengine yanafanyiwa kwa muda mfupi lakini baadaye manyanyaso yanaendelea na matatizo mengine pamoja na maslahi yote ya Bunge. Wewe kama Naibu Spika unaingia awamu ya pili, umejipangaje kumshauri Mheshimiwa Spika ili aweze kutoa tamko rasmi ambalo litawenza kuwalinda Wabunge, maslahi na manyanyaso wanayoyapata njiani?

SPIKA: Mheshimiwa Mgombea, majibu ya swali hilo.

MHE. DKT. TULIA ACKSON: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa ya kujibu swalii la Mheshimiwa Musukuma. Ameeleza kwa kirefulabda nisirejee kwa sababu wote tumesikia. Kama alivyosema, mimi kama msaidizi wako pia ni mshauri wako kwa changamoto zote ambazo Waheshimiwa Wabunge wanazipata huko barabarani na mengineyo aliyojasema, nadhani Mheshimiwa Musukuma ukiacha hili la barabarani ambalo amelielekeza moja kwa moja yale mengine ulishayasemea wakati ukigombea na Wabunge maadam walikupa kura naamini yataaka sawasawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hili la Waheshimiwa Wabunge kupata changamoto barabarani lina pande mbili; uko upande ambao sisi Wabunge kama raia wengine wowote tunaweza kufanya makosa barabarani. Kwa hiyo kwa muktadha huo lazima sisi kama Wabunge tuoneshe mfano mzuri wa kufuata sheria barabarani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pale ambapo pengine changamoto hizo zinatokea kwa namna ya kutuchelewesha kwenye shughuli zetu za Kibunge, hilo tutalifanya kazi na kila Mbunge atakuwa huru kabisa kuja kutoa taarifa, ama kama hakuweza kuja basi atatutaarifu hata kwa simu ya Mheshimiwa Spika, huwa iko wazi na ya kwangu pia huwa iko wazi, akitutaarifu sisi tutafuutilia ni jambo gani ambalo linamchelewesha kuwahi kwenye majukumu. Hata hivyo, tunatamani Mbunge asiishie barabarani kwa ajali kwa sababu alikuwa anafanya labda jambo ambalo haliruhuswi kisheria. Kwa hiyo niwaombe Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kuwa msaidizi wa Mheshimiwa Spika, nitakuwa namshauri yale mambo ambayo lazima zile sheria tulizozitunga wenyewe tuzifuate. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana, nakushukuru sana, sasa unaweza ukaenda kukaa. Tunakushukuru sana. (*Makofii/ Vigelegele*)

Katibu, sasa hatua inayofuata ni nini? Sijui idadi ya Wabunge tunayo tayari?

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

Mheshimiwa Spika, tunayo idadi ya Wabunge 350 mpaka sasa hivi, na kwa ruhusa yako tuanze kugawa karatasi kwa ajili ya zoezi la kupiga kura.

SPIKA: Ahsante. Wanaogawa karatasi sasa twende haraka. Tungeweza kuongezeka hata idadi tunaogawa karatasi ili tuokoe muda na wale wanaokuja na maboksi nao wajiaandae kufuatia muda siyo mrefu.

(Hapa Wabunge walipiga kura kumchagua Naibu Spika)

SPIKA: Twende haraka.

Maboksi yote yarudi sasa. Haya, maboksi mnayaona. Naomba Mheshimiwa Anastazia Wambura ufuatane na vijana hawa mwende mkatuhesabie hizi kura, tafadhalii tunakuomba. Haya, timu ya Katibu mnaweza mkaenda sasa.

Wakati wanakwenda kuhesabu kura, naomba niwatambulise kwenu wageni wa Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, wakiongozwa na Ndugu Leonida Lubala ambao wametoka kule Ilemela, Mwanza; wako saba. Wale wageni kutoka Ilemela; karibu sana wapendwa. Karibu sana na hongera sana kwa kuchapa kazi huko Ilemela; karibu sana watani zangu. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Geofrey Mwambe kutoka Masasi Mjini, wageni hao ni Ndugu. Gerald John Chamunda, Kelvin Rajabu, Rajabu Nampoto na Dionis Mwihumbo. Pale mlipo wale wa kutoka Masasi. Wale kule; karibu sana wageni wetu. *(Makofi)*

Sasa Waheshimiwa Wabunge wakati kura zinahesabiwa, niwape matangazo madogo madogo kadhaa; mojawapo ni kwamba, naomba tusikilizane, wale wenye magengemagenge kule nyuma naomba tusikilizane, naomba mkae Waheshimiwa Wabunge; hatutachukua muda mrefu, tutapata muda tu wa *ku-rub shoulders*.

Kwa kawaida Mkutano wa Kwanza kama huu tunakuwa na *free sitting* kama mlivokaa, lakini kuanzia Mkutano unaokuja huwa tunawapanga kwa majina. Sasa wakati mwingine tunaweza tukakupangia mahali ambapo hupapendi kabisa na kadhalika. Nilikuwa nafikiria sijui tufanye utaratibu gani ambao ungeweza ku-*indicate* kwamba ungependa kukaa wapi. Inanipa shida kuona tunafanyaje kwa sababu baadhi yenu mkiteuliwa kuwa Mawaziri basi mtalazimika kuja viti vya mbele hapa, kwa hiyo uki-*indicate* sasa hivi itakuwa ni tabu kwetu. Kwa hiyo hii sijui tu-*indicate* tutakaporudi? Maana yake wakati huo Baraza litakuwa liko kamili. Kwamba tuache *day one* ya Mkutano ujao iwe *free sitting* ili hapo utakapokaa wakati huo basi pawe ndiyo *permanent* hapohapo; nadhani itatusaidia zaidi. (*Makofii*)

Pia tulizungumza habari ya Kamati, zile fomu msisahau kuzijaza mki-*indicate preferences* zenu zote tatu na ya akiba, itatusaidia sana katika kujaribu kupanga uwe kwenye Kamati gani.

Mahudhurio ya Bungeni ni muhimu sana Waheshimiwa Wabunge. Mahudhurio ni moja ya matakwa ya Kikanuni. Kuhudhuria Mikutano na Vikao vya Bunge ni jambo ambalo hatutapenda kuwa tunakumbushana mara kwa mara. Tukumbuke kwamba tuna mitambo ya kila aina ya kujua mahudhurio yako na tuna-*keep records*.

Kwa kwa kuwa safari hii chama kikubwa ndicho chenye wajumbe walio wengi sana ni rahisi kweli ku-*control* nidhamu ya hilo; ni kupeleka tu kwenye chama kule kwamba hawa ndiyo watoro na tunajua *consequences* za hilo, kwa sababu wananchi hawakutuchagua tuje tuwe watoro, wametuchagua wakiamini tunakuja kuwawakilisha hapa. Kwa hiyo tujitahidi sana, tunajua kuna udhuru na nini, Mbunge ana mambo mengi sana, ana shughuli nyngi sana, hilo tunalitambua, lakini kadri iwezavyo basi jitahidi kuhudhuria Vikao vya Kamati, Mikutano ya Kamati, Mikutano ya Bunge, Vikao vya Bunge na kwengine kote tutakakokuomba uweze kuhudhuria.

Makatibu, naona Wabunge wangu wanavaa mikanda hii, kama sipendi hivi. Hebu Bunge ijalo mtafute namna ambayo inaweza kuwa lakini isiwe mikanda, kwa sababu mikanda ni ya wageni na Wabunge hawa ndio wenye nyumba yao hii, kwa hiyo tutafute namna na Waheshimiwa tupendekeze pia namna kwa Makatibu wetu hawa. Nafikiri kwa sababu ya mwanzo huu, walikuwa hawajui nani ni nani ikabidi watumie mikanda, mtusamehe kidogo, lakini kuanzia Bunge ijalo utaratibu huo wa mikanda hatutakuwa nao. Tufikiri namna bora zaidi ya kuwatambua Waheshimiwa Wabunge. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyowaambia jana, Mheshimiwa Rais anakuja kesho asubuhi hapa, *by* saa tatu tuwe tumekaa. Kutakuwa na gwaride linaloendelea hapo nje na shughuli nyingine za kumpokea, *by* saa nne kamili hotuba yake itaanza. Ni hotuba muhimu sana, nawaomba tuwahi, tuwepo na tuweze kufuatilia hotuba hiyo muhimu sana. Kama niliviyoshauri, kuanzia saa mbili hivi, ni vizuri uanze kuwasili hapa kwa sababu kwa kweli barabarani huko huwa kunachafuka na barabara za kuja hapa ni chache.

Hizi chaguzi kama tulizofanya leo zitaendelea sana tunakokwenda, tuna chaguzi za mara kwa mara; tutakuwa na chaguzi za Wenyeviti wa Bunge, tutakuwa na chaguzi za Wabunge watakaotuwakilisha kwenye Mabunge mbalimbali; Bunge la Afrika, Bunge la SADC, Bunge la Maziwa Makuu, Bunge la Afrika Mashariki itakapofikia wakati wake, yaani chaguzi zitakuwa nyingi tu huko tunakoenda. Kwa hiyo ni vizuri tujifunze kujua kuna fursa gani zinazokuja huko mbele kama unaona una sifa zinazofanana na kutuwakilisha huko, basi fursa hizo zitakuwepo. Usijione kwamba wewe ni Mbunge mpya au mgeni au nini, hapana, hakuna mgeni wala mwenyewji, kila Bunge linajitegemea. Hili la Kumi na Mbili lenyewe tu, halijawahi kuwepo la Kumi na Mbili wala halitakuwepo baada, ni sisi tulioko hapa, sote sisi ni seti moja tu. Kwa hiyo tuangalie, tujifunze, tujue ni vitu gani viro.

Tutakuwa na chaguzi kwenye Kamati za Uongozi wa Kamati, Wenyeviti, Makamu na kadhalika. Tulikuwa na

chaguzi za Spika na Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia, baadaye tutatangaza matokeo. Tunawashauri Waheshimiwa Wabunge na kwenye halmashauri zenu mnakoenda huko, utaratibu huu ni vizuri pia tukau-*adopt*. Si vizuri sana Meya wa Jiji mwanaume na Naibu Meya mwanaume. Hata kama haikuandikwa popote; katika nchi siyo lazima kila kitu kiandikwe, vipo vitu haviandikwi tu lakini inakuwa ni desturi, Rais mwanaume, Makamu mwanamke. Sasa ninyi hamuoni hivi vitu? (*Makofi*)

Lile Bunge lingine, Mama Makinda alikuwa Spika, mimi nilikuwa Naibu; hivyo na Bungeni hapa ndio tulikuwa tunaonesha njia kwa kuonesha mifano. Sasa katika halmashauri zetu hizo kama kuna waliogombea katika *categories* za namna hiyo, basi nadhani ni vizuri hilo nalo likatazamwa ili kuzoea kuwa na uongozi wa pamoja. (*Makofi*)

Pale ambapo wamegombea wanawake watupu au wanaume watupu ni suala lingine, lakini mahali penye mchanganyiko ni vizuri tukaweka taratibu zinazokwenda hivyo, inasaidia. Japo hatujatunga sheria wala nini lakini ni vizuri kulitazama jambo hilo.

Waheshimiwa Wabunge, zile Kamati tutakazoiunda zinategemeana na ndiyo maana hatuundi Kamati sasa, tunaunda Bunge Ijalo kwa sababu lazima tusubiri Mheshimiwa Rais ataunda Serikali yenyeye sura gani, kwa maana ya Wizara mbalimbali. Sasa ile namna atakavyoiunda Serikali, maana anaweza akapunguza, akaongeza Wizara mbalimbali, ndiyo inatuongoza sisi kuunda Kamati. Ndiyo maana Kamati zetu tunaziita Kamati za kisekta, zinaangalia Wizara ambazo zinaendana na sekta fulani kutegemea na Serikali jinsi ilivyoundwa. Kwa hiyo ndiyo maana tunazitengeneza Kamati zetu kwenye Bunge Ijalo kwa sababu Serikali itakuwa imeshajulikana, imeshatengenezwa. Mawaziri watakuwa wamekwishapatikana na kuapa, inakuwa haina tatizo.

Kuna vyama ambavyo bado havijaleta Wabunge japo wana fursa hizo hasa Wabunge wa Viti Maalum maana

tuna makundi matatu bado. Tuna Wabunge watano kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar ambao tutawapata tu kwenye Mkutano ujao wa Bunge kwasababu ndiyo wanakutana baadaye watachaguana kupata watano wale ambao Kikatiba wanakuja hapa. Halafu tuna kundi la Wabunge 10 wa Mheshimiwa Rais wanaoteuliwa nao tutawapata kwa kadri ambavyo Mheshimiwa Rais anaona sasa ni wakati wa kumleta Mbunge ye yote yule wa kumteua katiak nafasi zake zile za Kikatiba, nafasi 10 halafu tuna Viti Maalum kwa kuitia vyama nya siasa.

Viko vyama ambavyo havijatuletea Wabunge wao, tunachoona kwenye mitandao na mahali pengine eti wanalumbana, eti wasiwalete, sijui wawalete, yaani ni ajabu, ni aibu kubwa sana kwanza kwa vyama nya namna hiyo! Ndiyo hawa tunaosema, kwasababu ni fursa ya akina mama, wanalumbana wasije, wangkuwa hizo nafasi zina wanaume wangeshafika siku nydingi hapa, hao hao. (*Makofii*)

Sasa wapiga kura akinamama nchi nzima ndiyo mzidi kuvielewa hivi vyama hivi, shida! Wewe unawazuiaje akinamama wasije kutetea Watanzania humu ndani? Ni jambo ambalo halikubaliki kabisa. Kwanza haipasi kuwa hata ni mjadala lakini sasa ndiyo tuzidi kuwaelewa. Tunawaambia tu Februari hii tunaanza. Tukianza kwa utaratibu huo, madongo yake yatakuwa mazito. Wajitahidi mambo mengine mengine wapunguze kidogo. Viko vitu sio nya kubishania kwasababu ile ni fursa ambayo ni vizuri kuitumia. Mkiitupa, vyema! Wala hakuna shida kwa sababu hapa tunayo *quorum*, tuna kila kitu tunaendelea kama kawaida.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyowatambulisha Benki ziko hapa za kila aina, zinatupa kila aina ya ushirikiano. Mwenye nia ya kukopa, kwakweli wana *facility* za kila aina. Twende huko. Nawaonya kabisa, asije mtu Mbunge mwenzako akakuambia umkopeshe, yaani kabisa, nasema hili kutoka moyoni, sitanii. Utakuwa umeingia mkenge ambao hujawahi kuuona. Kuanzia wakati huo unashangaa urafiki umeisha, mnakutana kwenye *corridor* watu wamenuna, kesi zinaanza kwa Spika, oh huyu bwana, yule... nimeamua sana

mwaka jana kwenye Bunge liliopita. Safari huu bwana mtu akija tu naomba unikopeshe, mwambie bwana, unataka ugomvi na mimi? Tunaelewana jamanii? Hasa akinamama, Wabunge wanawake, mnakubali sana hivi vitu, vinawaletea shida sana, mno. Mpaka dakika ya mwisho mtu anatereza, inaanza kuwa homa kabisa. Usikubali, ukikopesha shauri yako! Kabisa wala usije kwa Spika wala kwa nani kwa sababu tumetoa tangazo hili mapema. Kwa sababu Wabunge sisi wote, shida yetu kubwa ni fedha, Jimbo linakuhitaji, kuna wagonjwa jimboni, watoto wa kusomesha, kwa hiyo, *we all need money*, lakini kurudisha inakuwa kidogo mtihani lakini watu wa Benki wao wana taratibu zao maalum ambazo ni vizuri tukaenda huko na tukapata mikopo yetu huko.

Mwisho nimtambulische mgeni wa Mheshimiwa Mwigulu Nchemba ambaye ni mke wake, Neema Mwigulu. Dada Neema yuko wapi? Sijamuona. Jamani mmemuona kule juu? Yuko juu kabisa kule, Neema hujaonekana bado. Ahsante sana Neema, ahsante kufika. Ahsante sana shemeji yetu. Amekuja kujitambulisha mapema kwamba jamani eh... Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

MATOKEO YA UCHAGUZI WA NAIBU SPIKA

SPIKA: Jamani nimekwisha pata matokeo kutoka kwa Katibu. Ni kwamba hakuna kura zilizoharibika. (*Makofi*)

Safari hii hili Bunge la wasomi watupu maana hakuna kura inayoharibika na tuliofiga kura humu ndani ni wabunge 354. Kura za hapana ni nne, kura za ndiyo ni 350. Kwa jinsi hiyo, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, amechaguliwa kuwa Naibu Spika kwa jumla ya kura 350. (*Makofi/Vigelegele*)

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. Nimeshamtangaza Mheshimiwa Naibu Spika wangu. Sasa nimuombe pale pale alipo basi atoe hotuba fupi ya shukranii. Ahsante sana. Karibu sana hapo hapo ulipo. Tena nimekosea kweli kweli hapo, lazima aapishwe, si ndiyo? Basi karibu sana hapa mbele kwa ajili ya kiapo. (*Makofi/Vigelegele*)

KIAPO CHA NAIBU SPIKA

*Hapa (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Aliapa Kiapo cha
Naibu Spika*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ahsante. Sasa tumruhusu Mheshimiwa Naibu Spika, Dkt. Tulia Ackson atoe salamu za shukrani kama anazo, ahsante karibu. (*Makofi*)

MHE. DKT. TULIA ACKSON - NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa fursa hii uliyonipa ya kutoa shukrani zangu baada ya kupigiwa kura na Waheshimiwa Wabunge. Ndugu zangu nimetoka hapa muda si mrefu kuwaomba kura, nichukue fur sa hii kuwashukuru sana kwa heshima hii kubwa sana mliyonionesha siku ya leo. Ni wazi heshimiwa hii si ya kwangu peke yangu, ni ya kwetu sisi sote kwa sababu nitakuwa mtumishi wenu nikimsaidia Mheshimiwa Spika kwenye nafasi hii. Pia niwashukuru sana kwa niaba ya wananchi wenzangu wa Jimbo la Mbeya Mjini kwa heshima hii kubwa sana mliyotupa siku ya leo ahsanteni sana.

Mheshimiwa Spika, na sisi tunawaahidi Waheshimiwa Wabunge kwasababu ninyi mnafanya kazi kwa niaba ya wananchi wote nchi nzima. Tunawaahidi kwamba tutafanya kazi kwa uaminifu tukimsaidia Mheshimiwa Spika ili tutimize majukumu yetu sisi kama Wabunge tunavyotarajiwa kuishauri Serikali, kuisimamia na wakati huo huo kuwawakilisha wananchi walioituamini mpaka sisi kufika hapa. Na mimi kama mtumishi wenu ninaahidi nitashirikiana nanyi katika yale yote ambayo mtahitaji niwasaidie nitawasaidia. Mkihitaji ushauri mimi nitawapa ushauri, lakini kwa yale mengine yote ambayo natarajiwa kumsaidia Mheshimiwa Spika, basi nitafanya hivyo kwa uaminifu.

Mheshimiwa Spika, ahsanteni sana kwa kura nyingi mlizonipa, ni wazo sisi sote ni Wabunge na sisi wote tungeweza kuwa katika nafasi hii ambayo mmeniheshimu kwayo mimi. Si kwamba mimi ni bora kuliko ninyi lakini ni wazi mmenitanguliza mbele yanu na mimi nitajitahidi kuwa wa mfano huko mbele ambako mmenitanguliza. Ahsanteni sana

Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana Mheshimiwa Spika, ahsanteni sana viongozi wote mlioko humu ndani na kwa n amna ya kipekee, ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Mwanasherini Mkuu wa Serikali. Ahsanteni sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru sana unaweza ukarejea kwenye kiti chako sasa. (*Makofii/Vigelegele*)

Ahsante sana. Sasa Waheshimiwa Wabunge, kwanza nisije nikasahau. Ni vyema hata shughuli zetu zikiisha kesho, unajua wiki ijayo tuna seminar lakini si vizuri kuondoka hapa *weekend* kwa sababu inawezekana tukapata ratiba ya kumuapisha Mheshimiwa Waziri Mkuu Chamwino, Ikulu. Hatujapata bado lakini inawezekana tukaipata ikawa hapo kati kati. Ni vizuri Waheshimiwa Wabunge wote tukawepo ili tuweze kuhudhuria hafla hiyo kwa sababu zoezi hilo ni muhimu sana kwetu sisi kama Wabunge. (*Makofii*)

Wakienda wenzetu wengine halafu sisi Wabunge hatupo, sisi lazima tujaze hilo hema la waalikwa, si ndiyo jamani? Mkiweza kuwepo basi litakuwa jambo la furaha sana.

La pili, kesho tutakuwa na ugeni wa aina mbali mbali, *gallery* zetu zote zitajaa na kuna baadhi ya wageni ambao watalazimika kuingia katika ukumbi wa Bunge na kama mnavyojua kuingia hapa ndani inatakiwa ruhusa kidogo. Kwa hiyo nitamuomba sasa Mheshimiwa Mwanasherini Mkuu wa Serikali atusomee pendelezo la kutengua Kanuni ili tuweze kuendelea.

Mheshimiwa AG, tafadhali.

HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE

MHE. PROF. ADELARDUS L. KILANGI - MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, hoja ya kutengenua kanuni za Bunge ambayo inatolewa chini ya kanuni 1974(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la Juni, 2020.

KWA KUWA kesho tarehe 13 Novemba 2020, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atalihutubia na kulifungua rasmi Bunge la 12, kwa Mujibu wa Ibara ya 91(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 na Kanuni ya 32(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Juni 2020;

NA KWA KUWA amewaalika viongozi mbalimbali kuja kusikiliza hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati akilihiutubia na kulifungua rasmi Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano ya Tanzania

NA KWA KUWA, Kanuni ya 160 Fasili ya Kwanza zinaeleza kwamba wageni wanaoruhusiwa kuingia Bungeni watakaa maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili yao na kwamba inabidi Bunge litengue Kanuni hizi ili kuruhusu viongozi maalum walioalikwa na Mheshimiwa Spika, kuja kusikiliza hotuba ya Mheshimiwa Rais, kuingia ndani ya ukumbi wa Bunge,

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba Kanuni ya 160 Fasili ya kwanza itenguliwe ili viongozi wafuatao waingie ndani ya ukumbi wa Bunge.

Kwanza, Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Pili, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, tatu Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Nne, Mheshimiwa Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tano Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Tano, Jaji Mkuu wa Zanziba na sita Spika wa Bunge la Afrika Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono na Bunge zima. Nawashukuru sana. Pamoja na kuungwa mkono ni wajibu wangu kuwahoji, wanaoafikiana na hoja hiyo ya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

SPIKA: Basi maandalizi yataendelea ili kuweka sawa maeneo baada ya kuwa tumeahirisha shughuli zetu hapa ili tuuache ukumbi wazi kwa ajili ya maandalizi maalum kwa shughuli ya kesho asubuhi.

Tangazo, Waheshimiwa Wabunge, yako matukio yanayoendana na shughuli ambazo zimeandaliwa na Benki yetu ya *CRDB* kwa siku ya kesho tarehe 13 Novemba, 2020. Pamoja na ushiriki wa shughuli za Bunge, napenda kuwashirikisha kwenye mambo makuu mawili ambayo washirika wetu Benki ya *CRDB* ambao ndiyo wametupatia mabegi wanatuletea pia siku ya kesho tarehe 13 Novemba, 2020.

La kwanza katika matukio hayo mawili, wanaom ba ushiriki wetu katika ufunguzi wa mashindano ya mpira wa kikapu wa *CRDB Bank Taifa Cup*, binafsi nitakuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wa mashindano ya Kitaifa ya mpira wa kikapu yatakayofanyika kuanzia saa tisa kamili jioni katika viwanja vipyta vya mchezo huo katika eneo la Chinangali, karibu na uwanja wa ndege.

Tunaombwa sana Waheshimiwa Wabunge saa tisa jioni tuwe pale eneo la Chinangali karibu na uwanja wa ndege ambapo mashindano ya mpira wa kikapu ya Kitaifa yanayoitwa *CRDB Taifa cup* yataanza. Mashindano haya yanajumuisha vijana 900 kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara na visiwani. Hawa ni wapiga kura wetu hivyo nawaombeni sana mje mjumuike nami katika hafla hiyo.

Pamoja na mechis zitakazofanyika pia kutakuwa na burudani mbalimbali. Watoa huduma mbalimbali watakuwepo na ambapo Benki ya *CRDB* imealika wajasiriamali ambao watatoa huduma uwanjani hapo muda wote ikiwemo nyama choma, vinywaji na watakuwepo baadhi ya wasanii wetu maarufu wa muziki wa kizazi kipyaa akiwemo Ndugu Joh Makini watakuwa wakitoa burudani

pale uwanjani. Itakuwa ni jioni nzuri tu kuweza kujumuika na Wabunge wenzetu wote na wananchi wa Dodoma na wananchi ambao wanatoka sehemu mbalimbali za nchi yetu ambao watakuwepo pale kwenye viwanja vya Chinangali karibu na uwanja wa ndege. Hiyo ni shughuli ya kwanza jioni kuanzia saa 9 mpaka saa 12 jioni.

Iko shughuli ya pili ambayo ni muhimu zaidi. Benki ya *CRDB* imeandaa hafla ya mchaparo kwa ajili ya kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa kwenu itakayofanyika katika hoteli ya Morena kuanzia saa 12 kamili jioni kesho. Pia nitakuwepo kama Mgeni Rasmi, kutakuwa na burudani mbalimbali, Waheshimiwa wote mnakaribishwa. Sasa hata kama utakosa kufika Chinangali, kwenye mchaparo napo? Tunaombwa sana basi jioni ile tufike, tuone hafla za Kibunge zinakuwaje na kwakweli hafla hiyo ya kesho jioni imeandaliwa vizuri sana.

Pameandaliwa vizuri sana kwa heshima ya kuchaguliwa kwenu na tunatangulia kuwashukuru *CRDB Bank in advance* kwa *gesture* hiyo. Kwa hiyo, natarajia kila mmoja wetu atafika ili basi iweze kuwa Ijumaa njema. Natumaini nyote mtaitikia kufika uwanjani na baadaye kuja kwenye mchaparo. Kule uwanjani kama una *tracksuit* au nini, hata kama ukija kama ulivyovaa, haina tatizo kabisa, hakuna *restrictions* za mavazi. Jioni vilevile ni *free wear*, uje unavyoona inafaa, hakuna tatizo. Lakini ni vizuri kufika kwakwell, *ku-rub shoulders*, kufahamiana, unajua bado hatufahamiana sana, kupitia hafla kama hizi zinatufanya tujuane kwa ukaribu, kufahamiana, kutengeneza urafiki, undugu ujamaa kama ambavyo mwisho wa siku Wabunge huwa tunakuwa hivyo.

Basi, Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa shughuli zilizopangwa katika mpango wa shughuliza Bunge kwa siku ya leo zimekamilika zote, naomba tena kwa mara nyingine nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hatua aliyofikia, tupelekee salamu kwa mama na familia, tuko nawe kama tulivyosema, tumefarijika sana sasa ni hapa kazi tu. Lakini pia nimefurahi na kufarijika kumpata msaidizi, Naibu Spika katika jina la Dkt. Tulia Ackson. Kule Kenya wana neno

lao wanasema, nimepata mutu wa mkono, kwa hiyo, yeye sasa ni mutu wangu wa mukono, nakushukuru sana dada yangu mdogo wangu, ninaamini kabisa tutaendelea kuchapa kazi kama tulivyofanya mwanzo kwa ushirikiano mkubwa kabisa kabisa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, mkimuona yeye, mkiniona mimi mjue yote ni sawa tu wala hakuna tatizo hata kidogo.

Basi sasa kwa hatua hii naomba niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu juu ya alama, kesho siku ya Ijumaa tarehe 13 Novemba, 2020.

*(Saa 07.05 Mchana Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,
Tarehe 13 Novemba, 2020 Saa Tatu Kamili Asubuhi)*